# *Ishara Za Kuja Kwake*

Asante, Ndugu Littlefield.

2 Mnaweza kuketi. (Sikujua jinsi ya kuishughulikia.) Kwa namna fulani kurudi katika kanisa hili zuri usiku wa leo kunaonekana kama kuja nyumbani (Nami nilikuwa na majaliwa makuu ya kuliweka hili wakfu kwa kazi ya Bwana wakati fulani uliopita.), na kuwa hapa pamoja na Ndugu yangu mpendwa sana Littlefield na kundi lake hapa, na kurudi kwenye maskini Cleveland, Tennessee, ambako daima kuna kupeana mikono kuzuri, kwema, kwa furaha. Hakika najisikia vizuri kulihusu, usiku wa leo.

3 Nilipiga simu, ama, niliwasiliana na Ndugu Littlefield wakati fulani uliopita, naye akasema, "Ndugu Branham, vipi kuhusu kuja huku ukatuone tena?"

Nikasema, "Vema, Ndugu Littlefield, nitafurahia kufanya hivyo. Ninaondoka sasa, lakini nitakaporudi, yapata Aprili, nitawasiliana nawe."

4 Tukaingia kutoka Arizona, kisha tukashuka kwenda Florida, na ndio kwanza turudi, nami nikampigia simu usiku huo. Yeye na maskini mke wake wa thamani walikuwa tayari wameenda kulala, lakini mimi—mimi niko macho saa zote, kama wahudumu walivyo, na kwa hiyo nikawazia, "Vema, haitakuwa imechelewa sana kumwita mhubiri," mwajua. "Yeye ni—yeye kwa kawaida yuko tayari wakati wowote." Na—naye alikuwa, mke wake akajibu simu, naye karibu alikuwa mikononi mwa Morpheus, mwajua, yule mtukufu wa usingizi. Kwa hiyo alikuwa, nikamwambia ya kwamba nitakuja huku, Bwana akipenda, kwa ajili ya Jumamosi hii usiku na Jumapili asubuhi, na bila shaka ni majaliwa makuu kurudi.

5 Ninataka kutoa shukrani zangu kwa Moteli ya City View, na Moteli ya Lehi kwa uungwana wao ambao wanatuonyesha, pia, hapa mjini, hata kwa kutusaidia na vyumba. Na—na watu walio pamoja nasi, waliwapunguzia bei, na vitu kama hivyo, kwenye vyumba vyao. Mwajua, hapa pangekuwa ni mahali pazuri pa kuishi, hiyo ni kweli, wanapowatendea Wakristo namna hiyo.

6 Patakuwa ni mahali pazuri pa u—uamsho wa Kipentecoste wa mtindo wa kale uliotumwa na Mungu, sivyo? Hakika pangekuwa. Nikishuka kuja huku, na kuona hili ni Church of God, makao makuu, huku chini kidogo barabarani, nililiona kwenye mkono wa kulia, uwanja mkubwa wa kambi. Na—na pamekuwa ni mahali pazuri sana hapa, kwa hiyo ni mahali pazuri pa uamsho.

7 Nami nimekuwa nikichukua baadhi yake kupitia somo fulani katika ninii, nyumbani, hapa Jumapili iliyopita, yapata

Jumapili tatu zilizopita, naamini ndivyo sasa, nilihubiri moja ya ibada zangu za kawaida za Jumapili asubuhi, saa sita tu, mwajua, juu yake. Na—na hivyo ndivyo ilivyokuwa, saa sita, aminini hilo. . . Na kwa hiyo, si—siwezi kuanza chini ya yapata saa tatu, mwajua, na halafu baada ya kupashwa joto, na kuanza kwenda mbio, mnajua, ndipo basi huwezi, hujui mahali pa kusimamia. Hakuna breki kwenye—kwenye—kwenye Injili, mwajua, kamwe huna mahali pa kusimama. Kwa hiyo tulikuwa na wakati mzuri sana.

8 Na halafu Jumapili, ninaamini Jumapili iliyopita, tulichukua yapata saa zingine tatu, juu ya mafundisho ya Neno, juu ya siku gani tunayoishi, na nyakati tunazoishi. Na imekuwa ni jambo tukufu kwetu, kuona Maandiko yakizungumzia mahali tulipo, kurudi nyuma na kuleta unabii, kuonyesha yale waliyofanya, kile kilichopo sasa hivi, na kile BWANA ASEMA HIVI ilicho kwa siku za usoni, zinazokuja. Mnaona? Nasi tunajua ya kwamba ni kweli. Haliwezi kushindwa kamwe kwa sababu liko katika Neno, nalo Neno sikuzote ni sahihi.

9 Sasa, laiti tungalikuwa na wakati wa siku chache usiku, yapata siku nane ama kumi usiku hapa katika nchi hii ya kupendeza, na kulitangazia makanisa yote kwa ajili ya ushirika na kukusanyika pamoja, bali hatuwezi kufanya hivyo. Ninaenda sasa, mara moja Canada, pamoja na Wahindi, huko nyuma kabisa barani, mimi, mbali sana. Nami, msimu uliopita wa kupukutika majani nilikuwa pamoja na maskini mmishenari mmoja kutoka huko, nami nikaona ninii yake, alikuwa ametoka kwenye nyumba nzuri sana, lakini mikono yake na chini *hapa*, na pande zote, kote kulikuwa kwekundu, nami nikauliza ilikuwa ni nini. Ni mahali ambapo viroboto na kunguni walikuwa wamemwuma kutokana na kukaa na Wahindi huko nje. Unajua, inakubidi tu kuishi nao.

10 Mimi, huko Afrika ningekula, wakati, ninii tu, sioni jinsi ningeweza kufanya hivyo kamwe, ilibidi tu Mungu anisaidie, hivyo tu, bali huna budi kufanya hivyo kwa vyovyote vile, unaona. Na kwa hiyo, watu wanaofanya umishenari hupitia mambo mengi yasiyopendeza. Lakini inatubidi kuwa mambo yote kwa watu wote, tupate kuwaleta wengine kwa Kristo.

11 Nami nilimhurumia sana Eddie, na watoto wake vivyo hivyo pia. Na maskini Eddie Byskal na mkewe, mwanamke mzuri kutoka kwenye nyumba nzuri ya kupendeza, baba yake ana kampuni kubwa, na rais wake, na kadhalika, kisha wayatoe maisha yao namna hiyo, hakika inahitaji Mungu kufanya hivyo, Ndugu Littlefield, huko kweli ni kujitolea.

12 Nao karibu wote ni Wakatoliki kule, kwa hiyo wao—wao, akamleta Chifu pamoja na Wahindi wanne ama watano, nao wakaingia moja kwa moja uwanjani, Roho Mtakatifu akashuka moja kwa moja na kuwaambia watu hao, na kuwaponya papo

hapo. Na sasa, karibu waiteketeze pwani hiyo juu chini. Wao ni wavuvi wa kibiashara, nao wanaingia kwenye mashua zao na kuondoka, njia pekee uwezavyo kwenda ni kwa mashua, wanapanda juu kabisa kupita Vancouver kando ya Kisiwa cha Malkia Victoria. Nawe unapanda kuelekea Alaska, kufuatilia pwani hiyo huko juu, huko ndiko tunakoenda, kisha turudi huko Fort St. John kutoka kwenye barabara kuu ya Alaska, kisha turudi.

13 Halafu basi, nikija huku juu kuwatembelea, juu tu ya hapa hata Pines ya Kusini. Hiyo nafikiri, tarehe 6, 7, na 8, ama, 8, 9, na 10 ya Juni, na halafu, tarehe 11 na 12 pamoja na Ndugu Bigby, nina hakika ninyi, wengi wenu mnamjua, huko chini Columbia, ninaamini ndiko, Carolina Kusini. Na halafu, tutoke huko kwenda—kwenda Ikulu ya Ng'ombe huko Lango la Kusini, Los Angeles, ambapo tunatarajia mkutano mkubwa kule.

14 Na kwa hiyo tunaninii, kisha kutoka huko twende kupitia California tuingie Oregon, Washington, na halafu Anchorage, Alaska, kisha turudi, Bwana akipenda, kwa msimu huu wa kuchipuka basi, tukiona basi mahali Bwana atakapotuongoza. Hakuna mwongozo maalum wa kwenda kokote kule, kupanda tu Mbegu, hivyo tu, mpaka tutakapopata mwongozo wa kufanya jambo fulani. Bila shaka tunatumaini ya kwamba mtatuombea.

15 Sasa, mchungaji wenu mwema sana na mkarimu amenipa majaliwa ya kufanya shule ya Jumapili asubuhi, kwa hiyo nikawazia, usiku wa leo, tungewekea msingi wazo kwa ajili ya kuwaombea wagonjwa, usiku wa leo, na kuwaombea wagonjwa, kisha asubuhi tuwe na somo la shule ya Jumapili.

16 Sasa, hilo ni zuri, wakati mtu atatoa mimbara yake mara mbili mfululizo namna hiyo, kwenye ibada yake ya mwisho wa juma. Mungu ambariki Ndugu Littlefield, yeye ni ndugu Mkristo mzuri, mzuri sana. Na kwa hiyo tutakuwa tukiwatarajia ninyi msio na wajibu wenu asubuhi, mbona, tutembeleeni. Lakini niliwazia usiku wa leo ingekuwa vema kuwaombea wagonjwa, maana huenda kukawa na... Sasa, tuliufanya usitangazwe, ili kwamba... kanisa letu ni dogo. Alitaka kupata ukumbi wa mikutano, Ndugu Littlefield anataka, nalo lingekuwa ni zuri sana kuwaleta watu wote. Nami nikasema, "Ndugu Littlefield, sina muda mrefu kutosha kukaa, ninii tu, hebu tuufanyie kwenye maskini kanisa lako."

17 Kuna jambo fulani kuhusu kanisa ambalo ni takatifu. Na—napenda kanisa, nanyi je? Mwajua, ukienda kwenye kumbi hizi za mikutano, tunazithamini sasa, ni nzuri, na watu walioturuhusu kuzitumia, wadhamini na kadhalika, lakini angalieni mliyo nayo hapo, mna upotovu wa kila namna, burudani za kila namna za ulimwengu, nao pepo wachafu wanakaa mle. Mnaona? Nao hu—huletwa tu na pepo. Halafu

basi, ukifika kanisani, Roho Mtakatifu yupo, mnaona, na kwa hiyo ni ninii tu, ni kitu tofauti tu kuhusu, kuja kanisani.

18 Nawazia tu hapa kuhusu, nilikuwa nikiwazia leo, ama, hivi majuzi niliandika jambo fulani baadaye, nilipokuwa nikienda zangu Arizona, ambapo Bwa—Bwana alikuwa amenionyesha jambo fulani lilikuwa linaenda kutukia. Nami kwa kawaida huandika, nisipowazungumzia watu, vema, nisingeweza kusimulia yote anayoonyesha katika mambo hayo. Lakini sasa, Roho Mtakatifu, hii *hapa* Biblia, na, *hapa*, hii ndiyo nyumba Yake ambamo a—anakaa, na anaishi pamoja na nyinyi watu hapa, Naye anajua hili kuwa kweli:

19 Yapata majuma sita yaliyopita, asubuhi moja, nadhani yapata, nilikuwa nikienda zangu Arizona pamoja na Ndugu Sothmann na Ndugu Wood, wawili wa wadhamini wa kanisa maskanini huko Jeffersonville, ndipo nikaona ono la jambo la ajabu, kulikuwa na watu wawili, na wote wawili walikuwa kwa namna fulani wamejipamba vizuri, na wote wawili walikuwa wapiganaji wa namna fulani, walikuwa wamevaa nguo za kawaida, lakini kwa namna fulani walikuwa wapiganaji hodari, walitaka kupigana, nao walikuwa wanaoneana kinyongo wao kwa wao. Basi mmoja wao . . .

20 Walikuwa wameingia, ilionekana kana kwamba ilikuwa katika, New York, ningeweza kujiona nikishuka kule kuelekea kwenye—kwenye viwanja vya michezo, na kadhalika, ambamo ninahubiri sana. Basi ilionekana kana kwamba kulikuwako na shimo dogo, mahali pa mviringo namna *hii*, mahali walipokuwa wameingia, basi wakaanza kupigana, ndipo mmoja akamwua mwenziwe.

21 Nami nikaona, ilionekana kama kitu chenye unyevu, ama maji, halafu walikuwa, kilionekana kitu kama selofeni, ambayo iliwekwa juu ya miguu ya mmoja. Kila kitu kikatulia kabisa, na ilikuwa ni huzuni, walikuwa wameua, mmoja alikuwa amemwua mwingine katika ugomvi mkubwa. Nami nikawaza, "Vema, sijui hilo linamaanisha nini hasa, Bwana." Kwa namna fulani nikaliandika tu. Nami . . .

Nyote mnajua yaliyotukia hivi majuzi, wapiganaji wawili wa uzito wa kati huko New York, wakipigana vikali, ndipo mmoja akamwua mwenziwe, mnaona.

22 Naye ni mwema kweli, sivyo? Akitujulisha mambo haya. Bila shaka hiyo haininii . . . Sababu . . . Halikuonekana kama, lilihusu Kanisa, kwa hiyo nikaliachilia tu. Na ni ninii tu, muda mfupi uliopita, sikujua habari zake mpaka muda mfupi tu uliopita. Nami nilikuwa nikiwazia, "Naam, bwana, nami niliandika hilo kwenye kitabu changu kidogo pale," Mnaona? Hiyo, hiyo, kitu fulani . . .

23 Sikujua ilikuwa ni nini. Niliwaona wakishuka chini, bila shaka shimo hilo, kana kwamba waliingia mahali hapo, lilikuwa

ni ulingo walimokuwamo, nao wanapigania ugomvi mkubwa, ndipo mmoja akamwua mwenzake. Kwa hiyo ugomvi mwingine mkubwa, yote mawili katika ninii . . . Wakati—wakati riadha na michezo inapofikia mahali hapo, ni wakati wa kuachana nayo. Hiyo ni kweli. Tukio lingine la Kaini na Habili, mnaona, pale kuona ndugu akimwua ndugu. Lakini tuna furaha sana kwamba tunajaribu kuwarudisha ndugu kwenye imani waliyokabidhiwa watakatifu mara moja tu.

24 Sasa, kuna watu wanaosimama, nasi hatutaki kuwaweka kwa muda mrefu kupita kiasi. Nami nina Maandiko hapa ninayotaka kusoma, na muhtasari fulani ambao, hapa ndani, maelezo madogo ya kitu fulani, na Maandiko yaliyoandikwa ambayo ningetaka kuyazungumzia kwa muda mfupi. Na tukipenda, hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwanza, kwa maombi tu.

25 Na sasa kwa wale waliopo na wangetaka kukumbukwa katika maombi, waweza tu kumwinulia Mungu mkono wako na kusema, "Sasa, nikumbuke tu, Bwana." Anaona kila mkono, hawa vijana, wasichana wadogo, wavulana, vijana kwa wazee. Sote tunajua ya kwamba tunaukabili Umilele.

26 Baba yetu wa Mbinguni, tena usiku wa leo, tunakikaribia kiti Chako—Chako cha rehema, kwa kuwa tumealikwa na Bwana wetu kuja, akisema, "Mkimwomba Baba lolote katika Jina Langu, nitalifanya." Sasa, tunajua ya kwamba Maneno hayo ni kweli, kwa hiyo tunakuja kwenye kiti cha rehema wakati kingali kimenyunyiziwa Damu ya Bwana Yesu, ikilia, "Baba, wasamehe." Kwa kuwa, Baba, kweli tunatembea, wakati mwingine na kujikwaa, tuseme, kwa sababu tunatembea katika ulimwengu wenye giza, na yote tuliyo nayo ni Nuru tu ya Injili, Roho Mtakatifu, kutuongoza, la sivyo tungeanguka katika Umilele wenye giza bila tumaini, bila Mungu.

27 Lakini tuna furaha sana kwamba Wewe umeandaa njia kwa ajili ya wale ambao wameitwa kwenye Karamu ya Arusi. Na ni majaliwa jinsi gani, usiku wa leo, kukusanyika pamoja na kundi, hao watu walioketi sasa, ambao wamealikwa kwenye Karamu ya Arusi, wakivaa, wakijifanya tayari sasa kwa ajili ya Arusi ijayo, tunashukuru sana kwa ajili ya jambo hili.

28 Na kuna haja nyingi nchini usiku wa leo, Bwana, haja Kanisani. Uliiona hiyo mikono ya thamani na ulijua kitu kilichokuwa nyuma ya mkono huo, kilichotulia moyoni. Mungu, angalia chini ndani ya moyo wa kila mtu binafsi na ujibu haja yao, hilo ndilo ombi langu Kwako, Baba.

29 Tunakushukuru Wewe kwa ajili ya kanisa hili, na kwa ajili ya kuishi kwake kwenye utukufu. Wakati wa giza, hata hivyo linasimama kama mnara wa taa, taa ambayo imewekwa juu ya kilima inayotoa miali yake kote nchini, kusudi watu waliochoka,

wagonjwa kwa dhambi wapate kuingia na kukaa pamoja nasi kwenye Nchi iliyo bora zaidi.

30 Mungu, mbariki mchungaji wake, ndugu yetu wa thamani. Nasi tunaiombea halmashauri yake ya wadhamini, halmashauri ya mashemasi, na kila mshiriki na kila mtu anayeishi hapa pamoja na watu hawa, kwa ajili ya makanisa haya makuu kote humu nchini, Church of God na msimamo wake mkuu kimataifa, yote mawili. Na, Mungu, siku moja, tunaamini, wakati utakuja ambapo tutakuwa mmoja, tumeunganishwa pamoja katika nguvu za Roho Mtakatifu. Tujalie, Bwana. Panda Mbegu sasa katika mvua hii ya masika, ili wakati mvua ya vuli itakapoanza kunyesha itazaa Mbegu za Injili zilizoiva. Tujalie, Bwana.

31 Tubariki usiku wa leo, sasa, mtumishi Wako asiyefaa, tunapojitahidi kuzungumza kwa dakika chache juu ya Maneno haya yaliyo mbele zetu. Tunaomba ya kwamba Wewe utatupatia muktadha wa hili somo. Tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

32 Sasa, tungetaka ninyi kuninii. . .Katika hili, katika kuzungumza usiku wa leo, Ninajaribu kujenga kwenye Injili katika siku tunayoishi, Nuru ya siku hii kwa ajili ya uponyaji wa Kiungu, kwa kuwa ninaamini ya kwamba Mungu amemwaga Roho Wake, na hii ndiyo saa ya ukombozi kwa wale wanaoutafuta huo.

33 Katika Kitabu cha Yeremia, mlango wa 10, kifungu cha pili:

> *Bwana asema hivi, Msijifunze njia ya mataifa, wala msishangae kwa sababu ya ishara za mbinguni; maana mataifa hushangaa kwa sababu ya ishara hizo.*
>
> . . .*Msijifunze njia ya mataifa,* (Sasa. . .) *wala msishangae kwa sababu ya ishara za mbinguni;*. . . *mataifa hushangaa kwa sababu ya ishara hizo.*

34 Sasa, tungetaka kuzungumza juu ya somo la—la *Ishara Za Kuja Kwake.*

35 Nimeona, hasa sana kutoka kwenu, watu wa Church of God, hapa juu katika—katika Cleveland na karibu, nafikiri ni makanisa yao ambayo mimi huona kando ya barabara, nilipowazia juu ya somo hili, "Iweni tayari, Yesu Kristo yuaja hivi karibuni." Nafikiri huo kwa namna fulani ni m—msemo miongoni mwao.

36 Vema, sasa, tunajua ya kwamba Mungu katika nyakati zote daima, kwanza, kabla hajafanya lolote, kwanza anawaonya watu na kuwapa ishara ya kitu kinachokaribia ambacho kinakuja. Maumbile hufanya hivyo yenyewe. Hali ya anga hupata joto kabla ya majira ya kuchipua, hupoa kabla ya majira ya baridi kali, na, loo, tungeweza tu kuendelea na kuendelea tukisema hivyo, maumbile yote, kwa hiyo basi, inampasa Muumba wa maumbile kutoa kioja, ama ishara ya jambo fulani linalokaribia

kutukia, kwa hiyo linazifanya hukumu Zake kuwa *za haki*, kwa sababu unaonywa kimbele.

37 Sasa, kama mtu akipita kwenye taa ya kusimamisha, naye ameonywa wakati akija, nayo inakuwa nyekundu, sasa anajua vizuri zaidi. Sasa, kama hakuna taa hapo, basi ni kosa la huo mji, ama yeyote yule ambaye hana ubao wa kusimamisha, alipaswa kuuweka hapo.

38 Lakini Mungu daima atatoa ishara ya onyo, mnaona, kabla jambo fulani halijatukia. Nami ninaamini kwa moyo wangu wote, kwa kuwa nimekuwa nikichunguza kindani mwaka huu uliopita kuliko hapo awali, juu ya kukaribia kwa Kristo, kule kuja kwa Bwana. Sasa, hiyo ama ni kweli, au si kweli. Biblia ama ni ya kweli, au si ya kweli. Na hapana . . . Ninaamini tu Biblia.

39 Sasa, Mungu hana budi kuuhukumu ulimwengu, siku moja, kwa Kitu fulani. Na kama atauhukumu kwa kanisa, basi atauhukumu kwa kanisa lipi?

40 Kanisa Katoliki linasema, "Sisi *ndio*." La Kilutheri linasema, "Sisi *ndio*." La Methodisti lilisema, "Sisi *ndio*." La Baptisti lilisema, "Sisi *ndio*." La Kipentekoste lilisema, "Sisi *ndio*." Na kuna yapata *ndio* thelathini, ama arobaini, ama labda hamsini tofauti katika hilo *ndio*, mnaona, matawi yake. Kwa hiyo nani *ndiye*?

41 Sasa, kuna kuchanganyikiwa kwingi sana hapo, hata mtu asingeweza kuweka imani yoyote juu ya machafuko. Kama umechanganyikiwa kuhusu endapo msichana uliyetaka kumwoa atakuwa mwanamke mwema au la, afadhali uachane naye, vivyo hivyo na mwanamume. Huna budi kuwa na kitu cha kuwekea imani msingi.

42 Si muda mrefu uliopita, nikizungumza na kasisi fulani, alisema, "Vema," akasema . . . Nilikuwa nikimwambia kuhusu . . . yeye . . . mwanamke fulani aliyehudhuria kanisa langu, nilikuwa nimembatiza binti yake, naye alikuwa ameolewa katika familia ya Kikatoliki na alitaka kuwa Mkatoliki. Naye alikuwa tayari amebatizwa, kwa hiyo akaniuliza kuhusu, hivi nilimbatiza huyo msichana?

Nami nikasema, "Naam."

Kasema, "Je, ulimnyunyizia?"

Nikasema, "Nilimpa ubatizo wa Kikristo," mnaona, "kwa kumzamisha."

Akasema, "Unajua, kanisa Katoliki lilikuwa likifanya hivyo."

Nikasema, "Lini?"

Akasema, "Vema, katika, Yesu Kristo na mitume."

Nikasema, "Unasema hilo lilikuwa kanisa Katoliki?"

Akasema, "Naam, Bwana."

43 Nikasema, “Nipe historia kuonyesha hilo, kwamba kanisa Katoliki liliwahi kuwako kabla ya miaka mia sita na sita baada ya kifo cha mtume wa mwisho.” Nikasema, “Hivi hapa *Waanzilishi wa Nikea*, *Waliotangulia Nikea*, *Baada ya Nikea*, *Mbili* cha Pember, ama, uh, *Nyakati za Mwanzoni* cha Pember, *Babeli Mbili* cha Hislop, *Kitabu cha Wafia Imani* cha Foxe, loo, *Kanisa la Mwanzoni* cha Broadbent, historia zote takatifu nijuazo zilizoko hapa, nionyeshe ukurasa mmoja, wakati wowote.” Mnaona?

44 Akasema, “Unajaribu kubishana kwa msimamo wa Kimaandiko.” Kasema, “Hatujali kile, kwamba hicho ni nini, Mungu yuko ndani ya Kanisa Lake, sisi ndio Kanisa.”

45 Nikasema, “Kama ninyi ndio Kanisa Takatifu, basi kwa nini msidumu na yale Biblia iliyosema? Kama mkisema wao ndio walioliweka Kanisa katika utaratibu, nanyi mnaubadilisha.”

Kasema, “Tuna haki ya kubadilisha utaratibu wa Kanisa, Mungu alitupa hizo haki.”

46 Nikasema, “Basi, kama hao mitume walikuwa Wakatoliki, tuseme walikuwa, halafu basi, wakafanya mambo waliyofanya kwa utaratibu waliokuwa nao, afadhali muurudie utaratibu huo tena.” Hiyo ni kweli.

Akasema, “Mungu yuko katika Kanisa Lake, Mista!”

Nikasema, “Mungu yuko katika Neno Lake, sio tu katika Neno Lake, bali Yeye *ni* Neno.” Kweli. Yeye ni Neno.

47 Mungu ni Neno, “Hapo mwanzo alikuwako Neno, huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alidhihirishwa, akakaa miongoni mwetu.” Papa hapa miongoni mwetu, Neno la Mungu, Mbegu Iliyonenwa, kutoka kwenye bustani yenyewe ya Edeni, wakati “kila mbegu itazaa kwa jinsi yake,” hiyo ni kweli, wakati Hawa alipopotoshwa, akasikiliza uongo wa ibilisi, na kuchukua mbegu mbaya katika tumbo la uzazi la nafsi yake kuamini Neno moja lililopotoshwa.

48 Usitake kupotosha Neno lolote la Mungu, sema tu kile Biblia ilichosema. Biblia ilisema ya kwamba *Hili*, hakuna unabii unaofasiriwa apendavyo mtu fulani. Kwa nini? Unabii ulitolewa na manabii, nalo Neno la Bwana liliwajia manabii, wanalifasiri jinsi tu lilivyokuwa, kwa hiyo hakuna ubishi Nalo.

49 Halafu basi katika Ufunuo 21 tunaona ya kwamba Mungu alisema, ama, 22, ninaamini ndipo, lilisema, “Kila atakayeondoa, au kuongeza katika unabii wa Kitabu hiki,” kwa hiyo ni Neno la Mungu kabisa, nao ulimwengu utahukumiwa kwa Neno hili, kwa hiyo hatutaki kulipotosha. Hatutaki kulifanya liseme chochote zaidi, ama chochote pungufu, liseme tu jinsi lilivyo, na kuliamini namna hiyo, nami niliona ya kwamba litazaa hasa, kwa sababu “kila mbegu itazaa kwa jinsi yake.”

50 Sasa, kama Hawa, sasa, yeye hakulikataa, alikuwa akitafuta hekima. Naye ibilisi daima anajaribu kuweka tafsiri ndogo ya kibinafsi, hekima kidogo juu ya Neno, “Linamaanisha *hivi*, ama linamaanisha *vile*.” Linamaanisha kile hasa Mungu alichosema lilimaanisha, na kwamba, liseme tu namna *hiyo*, na hilo latosha. Hivyo ndivyo ninavyoliamini, nami ninajua ya kwamba ni kweli, kwa sababu Yeye hulidhihirisha na kuthibitisha kwamba ni kweli. Mnaona?

51 Sasa, kama upotosho mmoja mdogo wa Neno la Mungu ulisababisha kila mauti, kila sononeko, kila huzuni, kila kitu, shida ambazo tumepitia, kupotosha tu Neno moja dogo la Mungu, nao hawakuepuka, imetugharimu miaka elfu sita ya huzuni, na hata Mwana wa Mungu kuja duniani apate kufa kuikomboa jamii ya binadamu, kila vita, kila huzuni, kila mama asiyeolewa, kila kitu kibaya kilichopata kutokea ulimwenguni kilikuwa ni kwa sababu ya mtu mmoja kutokuamini, aliamini tisini na tisa na asilimia tisini na tisa ya Neno la Mungu, na kupotosha tu kidogo, kidogo sana mwishoni, na kusababisha haya yote, basi upotovu mmoja mahali popote, usifikiri kamwe utarudi, chochote pungufu ya Neno lote la Mungu. Liamini, simama juu Yake, hatuna budi kusema kama tu lilivyosema.

52 Kwa hiyo Mungu huwakaribia watu Wake kwa ishara na maajabu. Sasa, “Msiziegemee njia za wapagani.” Sasa, *mpagani* kwa kweli, kwa tafsiri, ni “asiyeamini.” Mnaona? “Msijifunze njia ya wapagani,” asiyeamini, kaa mbali naye. Unaona? Usishiriki naye hata kidogo, yeye ni asiyeamini, hebu na atiwe alama kama asiyeamini.

53 Je, giza linaweza . . .? Je, nuru na giza vinaweza kuwepo kwa wakati mmoja? Je, kunaweza kuwa giza wakati jua linawaka? Hasha. Ni lipi lililo na nguvu zaidi? Giza laweza kulizima jua? La, bwana, jua huzima giza, mnaona, nuru. Hiyo ni kweli na uongo. Mnaona? Kwa hiyo makosa hayawezi kamwe kuwepo katika hali ya ukweli, na wala uongo hauwezi kuwepo mbele ya—mbele ya kweli. Ukweli daima ni ule ule, uongo hugeuzwa na bado ni uongo. Mnaona? Kwa hiyo ni ninii tu, ni kweli.

54 “Wala usijifunze njia ya asiyeamini.” Sasa, kama yeye ni asiyeamini, acha awe vile anavyotaka kuwa, lakini wewe kuwa mwaminio. *Mpagani* linamaanisha “asiyeamini,” mtu asiyeamini Nini? Loo, asema, “Ninamwamini Mungu.” Kama huliamini Neno la Mungu, basi humwamini Mungu. Hiyo ni kweli.

55 “Yeye asemaye ananipenda, asiyetii amri Zangu ni mwongo, wala Kweli haimo ndani yake.” Kwa hiyo basi, hatuna budi kuliamini Neno la Mungu, hilo linathibitisha tunampenda Mungu, tunapoliamini Neno Lake. Kama ukisema ya kwamba ulinipenda, wala hukufanya yale niliyosema, ama kutimiza neno langu, ama nilisema nilikupenda, na ni vinginevyo,

mbona, unaona, ingethibitisha kwamba hatukufanya hivyo, hatukuaminiana. Kwa hiyo vi—viumbe havina budi kumwamini Muumba, na kupitia hapo huleta muungano.

56 Ni kama tu kuchukua waya na kuuunganisha na da—dainamo ambapo kuna umeme, au kuchukua waya na kuichomeka kwenye soketi ambapo hakuna umeme. Unaona, ndiyo tofauti, ni waya tu uliokufa, haidhuru uko kwenye soketi kiasi gani, ungali, kama hamna umeme mle ndani, ungali ni waya uliokufa. Na mradi tunajaribu kuungana na kitu fulani, hauna Uzima wowote wala Kweli yoyote ndani yake, bado utakuwa ni ngurumo iliyokufa bila radi ndani yake. Hiyo ni kweli. Lakini hatuna budi kuunganishwa na Neno, Neno la Mungu, hilo ndilo Kweli ya Mungu.

57 Naye alisema usiiegemee njia yao, usijifunze njia zao. Kaa mbali nao, jitenge nao. Na kufadhaika, msifadhaike, kwa maana wanafadhaika. Kufadhaika hutokana na neno *kuvunjika moyo*. Ni kitu gani? Asiyeamini amevunjika moyo. Na nini? Ishara za Mbinguni. Inamfanya tu asiyeamini, kuvimba tu kwa hasira, unapozungumza juu ya ishara na maajabu na kadhalika, hawaamini hilo. Ukianza kuzungumza juu ya uponyaji wa Kiungu, "Loo, kanisa letu halifundishi hivyo, sisi—sisi, mbali na hilo." Ubatizo wa Roho Mtakatifu, "Loo, huo ulikuwa tu kwa ajili ya mitume pekee." Mnaona? Usijifunze njia zao, usiwakaribie, jifunze Neno, dumu na Neno. Neno ndilo Kweli.

58 Sasa, usijifunze njia zao, kwa sababu wanafadhaishwa na ishara za Mbinguni. Hivyo ndivyo hasa Biblia ilivyosema hapa katika Yeremia mlango wa 10 na kifungu cha pili, na kirai cha mwisho cha kifungu hicho, kilisema, "Zinawafadhaisha." Zina—zinawavunja moyo. Wananinii tu, zinawavunja moyo.

59 Sasa, kama zinawavunja moyo, hizo ishara zinawavunja moyo na kuwafadhaisha, zinamtia moyo mwaminio. Naam, hiyo ni kweli. Ati nini? Inamkatisha mtu tamaa. Kwa sababu gani? Anaamini Neno, Hilo ni . . . kumtia moyo mwaminio katika kweli ya Kimaandiko. Ishara, mnakumbuka, ninazungumza juu ya ishara za kuonekana Kwake katika kizazi hiki. Sasa, ndipo basi, kama tunaweza kuonyesha hapa katika Maandiko ya kwamba *hiki* ndicho kizazi kitakachoona kuja kwa Bwana, basi, ama, tutaninii tu . . . hii . . . Nini?

"Loo," ulisema, "Una hakika na hilo?"

60 Vema, mimi . . . Tutaangalia tu na kuona kile ishara zinaelekezea, mnaona, tuone jinsi tulivyo karibu. Kama kibao cha kuelekeza kinasema, "Unakaribia, umbali wa maili chache tu," afadhali uanze kujiandaa, kwa sababu huenda ikawa ni umbali wa saa chache tu, mnaona. Lakini Yeye alitwambia kile ambacho kingetukia kabla tu ya wakati huu, na hilo ndilo tutakaloangalia.

61 Sasa, kwa asiyeamini, yeye amefadhaishwa na ishara za Mungu za Mbinguni. Yeye, zinamvunja moyo, hataki kuziwazia, asingefundisha hilo kanisani mwake, asingewaruhusu watu wake kuliamini. Mnaona? Yeye—yeye—yeye amefadhaika, hataki kitu hicho karibu naye hata kidogo, asingemruhusu mhubiri mimbarani mwake, anayeamini hivyo. Hiyo ni kweli.

62 Nilikataliwa na kundi la Kipentekoste juma lililopita, ambapo maelfu ya barua zilimiminika, na kadhalika, kwa sababu walikuwa wamefadhaika. Mnaona? Hiyo ni kweli, Mpentekoste, si Mpresbiteri sasa, Mpentekoste, amefadhaika, iliwatia wasiwasi, kuhusu ishara za Mbinguni, maajabu yakitokea, wamefadhaika.

63 Lakini kwa mwaminio, ni thibitisho la kweli ya Neno la Mungu linalonena juu ya ishara inayokuja. Amina. Inathibitisha Neno la Mungu kuwa ni kweli, hiyo ni kwa mwaminio. Amina. Asiyeamini, ana wasiwasi, amefadhaika, amevunjika moyo, "Loo, kundi kama hilo!" Atasema, "Humaanishi wewe ni mfuasi wa kitu kama *hicho*?" Mnaona? Limemvunja tu moyo. Na, lakini kwa mwaminio, ni, loo, ni asali katika mwamba, ni thibitisho.

64 Siku moja nilikuwa nikisoma makala ndogo ya m—mtu ambaye—ambaye alienda huko . . . aliwapenda ndege weusi, naye alikuwa na sha—shamba lililojaa stroberi kwa sababu hao ndege weusi wanapenda stroberi, naye alipenda, kuona ndege wakija kila msimu wa kuchipua, na huko juu kaskazini. Nasi tuna stroberi tamu huko juu, sehemu ya kaskazini ya taifa letu.

65 Na kwa hiyo, akaondoka na kupaacha mahali hapo. Ndipo majirani wakaingia, nao wakawazia wangewafukuza hao ndege na kuchuma hizo stroberi, maana huyo mzee hakuwa anarudi, kwa hiyo akaweka kitisha ndege huko nje uwanjani.

66 Ajabu ni kwamba, wakitembea barabarani, wakati hao ndege weusi waliporudi, wakidhani wangeshiba mlo wa stroberi, kulikuwa na baadhi yao wameketi huko juu kabisa mitini, wakilia tu na kupiga makelele, hawa hapa wengine wameketi kwenye nyaya za simu, walikuwa wakilia, wengine wameketi kwenye nguzo ya ua, wakilia. Shida ilikuwa ni nini? Vurugu hizo zote, na kile walichokuwa wakililia, kulikuwako na stroberi nyingi sana, sio kwamba hakukuwako na stroberi, kulikuwa na mazao mengi, bali waliogopa kile kitisha ndege, hivyo tu.

67 Ndipo nikawazia, "Hivyo karibu ndivyo ilivyo kwa watu, hata hivyo, ibilisi ataweka maskini kitisha ndege huko nje, na kumtisha kila—kila hua nchini, akiweza, ama, kila tai, huenda nikasema, ikiwezekana. Naam, bwana. Ata—atafanya maskini kitisha ndege fulani na kumfanya kila mtu aogope, mnaona.

68 Na, lakini ilinishangaza, moja kwa moja kwenye mkono wa hicho kitisha ndege kulikuwa na ndege wawili wakubwa, wenye afya, wakila tu berinyeusi, ama, stroberi, pasipo kumjali mtu. Mnaona? Nami nikawaza, "Hiyo ni kweli. Hakuna hukumu

kwao walio katika shamba. Hilo ni jambo moja, hakika." Naam, bwana. Wao, mbona, hawakukijali hicho kitisha ndege hata kidogo, waliketi pale pale na kula vile vile tu, kwa sababu zilikuwa ni stroberi, nazo zilikuwepo kwa ajili yao.

69 Basi Mungu ambariki mwanamume au mwanamke huyo, anayeweza kutembea kando ya kila kitisha ndege kisichoamini, anayejaribu kuelekeza kitu *hiki* ama *kile*, aingie moja kwa moja shambani, kwa sababu kuna Zao zuri, amina, moja kwa moja katika msimu wake, ingia moja kwa moja shambani sasa. Hakuna hukumu kwa hao ndege wakubwa ambao wanaweza kuingia moja kwa moja mle ndani wala hawaogopi kitisha ndege.

70 Thibitisho la Neno la Mungu kuwa ni kweli, Mungu hushuhudia Neno Lake kwa ishara Zake. Neno la Mungu ni Mbegu, na Mbegu hiyo haina budi kuzaa kwa jinsi Yake, Mwanzo 1:11, "kila mbegu kwa jinsi yake." Naye Yesu alisema ya kwamba Neno la Mungu lilikuwa ni Mbegu ambayo mpanzi alipanda. Kwa hiyo basi, kila ahadi katika Biblia haina budi kuzaa kwa jinsi yake. Amina.

71 Sasa, utaliepukaje? Wanaposema hakuna Kitu kama Roho Mtakatifu katika siku hii, kwamba alitolewa tu kwa mitume, wakati Petro aliposema kwenye Siku ya Pentekoste, wakati wote wangempokea Roho Mtakatifu, sasa, angalieni walichokuwa wakifanya, kulingana na Isaya na manabii wote waliotabiri kwamba Roho Mtakatifu angemwagwa, sasa, huyu hapa mtu chini ya uvuvio wa Roho Mtakatifu, alisema, "Ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa watu wote walio mbali, hata wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie."

72 Sasa, kama unaogopa vitisha ndege, kamwe hutaipata. Unaona? Lakini kama huogopi, njoo moja kwa moja nyuma ya kitisha ndege, haidhuru ni kitu gani kimesababisha *hili* na *lile*, hilo halina uhusiano wowote nawe wala na Neno la Mungu, dumu tu moja kwa moja na Neno.

73 Sasa, ishara ni thibitisho la Neno la kweli. Mungu katika nyakati zote amefanya hivyo. Sasa, baadhi yenu huenda mkataka kuandika baadhi ya Maandiko haya, ikiwa mnataka, wekeni Waebrania 2:4 hapo. Mnaona ya kwamba Mungu amewathibitisha, amewathibitisha wajumbe Wake, "Mungu kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi," Waebrania inaanza, "alisema na baba zetu katika manabii, katika siku hizi za mwisho kupitia Mwanawe, Kristo Yesu." Mnaona? Na kuona kwamba hao walihubiriwa Injili zamani za kale, na walikuwa na ishara na maajabu kuthibitisha hilo, basi ni zaidi sana vipi inavyotupasa kumshikilia Mungu kwa ishara mbalimbali na maajabu na karama za Roho Mtakatifu? Loo, ishara mbalimbali, ishara ambazo Yesu Kristo alionyesha kwamba alikuwa hapa duniani, Yeye alikuwa ni Nani, na kile alichokuwa, na ninii—na kilichomleta hapa.

74 Si ajabu Yeye alisema, "Mnaweza kuutambua uso wa mbingu, bali ishara za wakati hamwezi kuzitambua. Kama mngalinijua Mimi, mngaliijua siku Yangu." Hiyo—hiyo ndiyo shida siku hizi, watu wanatambua . . . wanakosa kuitambua siku tunayoishi. Mambo haya hayana budi kuwa hivi, hakuna kitu kilicho nje ya utaratibu, kila kitu kinaenda kikamilifu.

75 Nilihubiri si muda mrefu uliopita juu ya somo dogo, Waebrania, samahani, Mathayo 11:6, ni, nililiita, naamini, *He—He—Heri Iliyofichwa*. Ilikuwa ni Yesu akinena, wakati wanafunzi wa Yohana walipomjia, mwajua, na kusema . . .

76 Yohana alichoka kidogo kule chini, kwa sababu alikuwa amehubiri ya kwamba kulikuwa na Kristo anayekuja (Sasa, hili lingekuwa zuri kwa ndugu wa Kipentekoste.), kulikuwako na Kristo anayekuja. Yohana alisimama huko nje na shoka lililowekwa penye shina la mti, huku nyoka wakikimbia. Hivyo ndivyo alivyofundishwa, alikuwa nyikani, hakuwa na ujuzi wowote wa seminari, kwa hiyo kitu pekee alichojua kilikuwa ni shoka, na nyika, na kundi la nyoka. Na hivyo ndivyo alivyofananisha kila kitu, mnaona, kile alichokuwa ameona nyikani. Na kwa hiyo a—alijua ya kwamba ilimbidi nyoka kutoroka anapofukuzwa.

77 Kwa hiyo basi akawaambia Mafarisayo, "Enyi wazao wa nyoka, ni nani aliyewaonya kuikimbia ghadhabu ijayo," mnaona. Kwa hiyo akisimama pale nje alisema, "Atausafisha sana uwanda Wake, ataikusanya ngano ghalani Mwake, Naye ata—ataifagilia mbali, kisha ayateketeze makapi kwa Moto usiozimika. Nalo shoka limekwisha kuwekwa penye shina la mti." Loo, jamani, ni Masihi wa jinsi gani ajaye!

78 Lakini basi, alipofika pale, Jamaa mdogo, mpole, mnyenyekevu, mabega yaliyoinama chini, Biblia ilisema, "Hana uzuri hata tumtamani. Mtu wa huzuni, ajuaye sikitiko."

79 Wakati Yohana alipoingia gerezani, alianza kuwaza juu ya haya yote, yale . . . Lakini akasema, "Nina hakika niliona ishara sahihi. Mimi . . . Sasa, sasa, Yeye—Yeye aliniambia huko nyikani, ambaye nitamwona Roho huyo akishuka na kukaa juu Yake, Huyo Ndiye atakayebatiza kwa Roho Mtakatifu na kwa Moto. Niliiona ishara hiyo, ninashuhudia hiyo ni kweli, Huyo ni Mwana wa Mungu. Lakini labda Yeye . . . Jamaa fulani akitenda namna *hii*, hapana shaka kuna kasoro, afadhali ni—niende nikachunguze." Akawatuma baadhi ya wanafunzi wake.

80 Yesu kamwe hakusema, "Sasa, ngoja kidogo, nitamtumia Yohana ki—kitabu ambacho ndiyo kwanza tupate kutoka kwenye seminari, jinsi ya kuenenda gerezani kwa ajili ya haki." La. Kamwe hakusema, "Mwambieni alipaswa kuchukua miaka miwili zaidi chuoni, kama baba yake alivyofanya." Kwanza kabisa hata hakuenda chuoni, hata hakwenda shuleni.

81 Baba yake na mama yake walikufa alipokuwa mvulana tu, kwenye umri wa miaka tisa akaenda nyikani, maana alikuwa na Ujumbe uliotoka kwa Mungu, si kutoka kwa kanuni fulani ya imani ya kujibunia. Yeye—yeye. . . Ilibidi itoke kwa Mungu. Siku za—za—za—zake zilikuwa muhimu sana asingeweza kujipumbaza tu na ujuzi mdogo wa seminari kama aliokuwa nao baba yake, bila shaka alikuwa ni kuhani. Wala kamwe hakuhudhuria shule ya baba yake, alienda nyikani, kusudi ahudhurie shule ya Mungu.

82 Naye Mungu akamwambia hasa, "Sasa, hili haliwezi kukosea, Yohana, huna budi kuingojea ishara hii, utakapoona ishara hii ikitokea pale, kama Roho Mtakatifu akishuka kama wingu la Moto, na mbawa za hua zikishuka, Huyo Ndiye."

83 Yohana akasema, "Nilimwona, bali Yeye hatendi namna hiyo, kwa hiyo nendeni mkaangalie."

84 Kwa hiyo Yesu akasema, "Nawaambia, msirudi bado, wala msichukue kitabu wala chochote kile." Akasema, "Kaeni tu mpaka ibada iishe, ngojeni mpaka ibada ya jioni iishe." Ndipo waliporudi, Yeye alisema, "Enendeni mkamwonyeshe Yohana." Amina. "Niko kwenye wakati ufaao kabisa, siko nyuma ya wakati, niko. . . kila kitu kiko sawa kabisa." Amina. Mnaona?

85 Hivyo ndivyo tunavyofanya siku hizi, tunafikiri jambo fulani limetukia, sivyo, Yeye yuko kwenye wakati mzuri, amina, hajachelewa hata kidogo, kila kitu kinaendelea sawasawa kabisa, moja kwa moja kwa wakati wake. "Enendeni tu mkamwonyeshe Yohana yale yanayotukia na kumwambia, 'Heri yeye, asiyechukizwa Nami.'"

86 Ndipo baada ya kuondoka. . . Ninapenda maoni hayo. Mnaona, Yohana alikuwa amemtolea Yesu moja ya matamshi duni sana, akamwuliza, "Kama wewe Ndiwe," mnaona. Lakini Yesu alijua hali yake, jinsi alivyokuwa ameteseka na kuwekwa mle gerezani, na kama vile Pember alivyosema, "Jicho lake la tai liliingia utando." Kwa hiyo nadhani, labda akiwa pale, karama yake ya kinabii haikuwa ikifanya kazi vizuri, alikuwa amekaa mle gerezani, akijua atakatwa kichwa chake katika muda mfupi.

87 Na, lakini Yesu aligeuka na kumpa sifa kuu sana ambazo mtu yeyote angeweza kumpa, Akasema, "Mlitoka kwenda kuona nini? Mlitoka kwenda kuona nini? Unyasi unaotikiswa na upepo wowote? Si Yohana. La, la." Kasema, "Je, mlienda kumwona mtu kutoka kwenye seminari aliyevaa koti rasmi, ukosi wake wa mviringo, unajua?" Akasema, "Hao wanaovaa nguo za aina hiyo ndio wa kuwabusu watoto wachanga, na mwajua, na kuoa vijana, na kuzika wafu." Kasema, "Wanazunguka kwenye majumba ya mfalme," na D.D., Ph., LL., QU., mwajua, na hayo yote, mwajua, na mnaona, "hao ndio. Lakini mlienda kuona nini? Nabii?" Akasema, "Nawaambia, na zaidi ya nabii." Naam, bwana.

88 Kasema, “Kama mnaweza kulipokea, huyu ndiye, aliyesema,” Malaki 3, “‘Namtuma mjumbe Wangu mbele ya uso Wangu, kuitengeneza njia.’ Huyo ndiye aliyekuwa.” Sasa, mnaona kulikuwa na ishara, alikuwa akiangalia ishara hiyo.

89 Sasa, sasa, Mungu katika nyakati zote aliwapa watu ishara, kulishuhudia, Kumbukumbu la Torati 18:22, pia 13:1, kama mkitaka kuandika Maandiko haya, Mungu aliwapa Israeli ishara iliyohakikishwa. Yeye alisema . . . Sasa, Mungu hulituma Neno Lake kwa manabii Wake. Hiyo ni kweli? Ni vile hasa Biblia ilivyosema, “Neno la Bwana liliwajia manabii.”

90 Alisema hilo lilikuwa ndilo jaribio la nabii: Kama nabii alitabiri, na yale aliyosema yatimie, basi msikieni, lakini lisipotimia, basi Mungu hajanena, hivyo tu, kwa hiyo msi—msimwogope. Hiyo ni kweli. “Akiwepo mmoja miongoni mwenu aliye wa kiroho ama nabii, mimi Bwana Mungu, nitajitambulisha Mwenyewe kwake katika maono, nitasema naye katika ndoto, na likitimia, basi Mimi, Huyo ni Mimi ninayenena.”

91 Hakika, Mungu hatasema uongo, mnajua Yeye hawezi kusema uongo, hakuna kitu ndani Yake cha kudanganyia. Yeye ndiye Chemchemi ya usafi wote, kweli yote, ni Mungu, kwa hiyo uongo hauwezi kutoka kwa Mungu, Yeye ni mkamilifu, safi.

92 Na kama ni Neno la Bwana, basi ni mawazo Yake aliyotafakari kimbele. Amina. Hivyo ndivyo tulivyo na Uzima wa Milele, kwa sababu tulinenwa na Mungu tukawa, sio kujiunga na kanisa, bali kuzaliwa kwa Neno, Mbegu ya asili, ambayo Mungu alisema, “Na iwe,” ikawa. Amina. Hivyo ndivyo Mungu anavyowazaa watoto Wake siku hizi, katika tumbo la uzazi la moyo wao kwa Neno Lake, nalo Neno Lake linatoa mizizi na kukua.

93 Roho katika moyo wa mwanadamu anawezaje kusema ni wa Mungu na kukana Neno hili, wakati Neno-Mungu Lenyewe Ndilo lililo ndani ya moyo wa mwanadamu? Amina. Kama sivyo, ni ninii, kitu kingine, halafu si Roho Mtakatifu mle ndani. Vema.

94 Sasa, manabii wa Bwana walitoa ishara na maajabu kwa kila kizazi. Manabii, manabii wa kweli wakiwa na Neno la kweli walitoa ishara za kweli za Kimaandiko. Sasa, kumbukeni, sasa, tunataka kutofautisha hapa kati ya mema na mabaya, kwa sababu, kumbukeni, katika, Biblia ilisema, katika Mathayo 24, ya kwamba zile roho mbili katika siku hii, ambazo tunafikia katika dakika chache, zingefanana sana hata zingewapoteza walio Wateule kama yamkini. Nina furaha ilisema, “*kama* yamkini.”

95 Wateule, bali wale walioteuliwa walijulikana tangu zamani na Mungu, “Wale aliotangulia kuwajua, aliwaita; wale aliowaita, aliwahesabia haki; wale aliowahesabia haki, tayari, amewatukuza.” Huo ni ukweli uliothibitishwa. Naam,

bwana. Kwa hiyo basi, mnaona, ingewapoteza walio Wateule kama yamkini, na bila shaka lilionekana kama jambo sahihi. Vema.

96 Sasa, lakini manabii wa kweli walitoa ishara za kweli za Neno la kweli (Hiyo ni kweli?), Neno la kweli. Hebu niwataje wachache tu, mmoja wao papa hapa, kabla tu hatujaenda mbele zaidi. Jinsi uongo unavyoweza kuonekana sana kama ukweli! Je, ninawapigia kelele sana? Hiyo ni, sauti hiyo ni kubwa sana? Angalieni, mnaweza kunisikia huko nyuma? Sawa, loo, sawa. Sasa, ni kweli jinsi gani . . . jinsi kweli na uongo zinavyofanana! Jambo ambalo Shetani alimwambia Hawa lilikuwa karibu ni kweli kabisa.

97 Angalieni, wakati, katika nyakati za Yehoshafati na Ahabu, Ahabu alikuwa amejihifadhia manabii mia nne wa Israeli. Sasa, wao walikuwa ni manabii, manabii wa Israeli, Wayahudi, katika mkondo wa ile kweli, manabii. Alikuwa na mia nne wa hao aliokuwa amewasomesha na kuwatunza.

98 Na kwa hiyo Yehoshafati akashuka apate kufanya mapatano na Ibra- . . . na Ahabu, basi alipofanya hivyo, akasema, "Je, twende Ramoth-gileadi, na kuiteka nchi hiyo?"

99 Vema, walisema na hao manabii. Kumbukeni, angalieni jinsi ilivyoonekana ya *kweli*: Hao manabii wakasema, "Kwea, Bwana yu pamoja nawe." Kwa nini? Walikuwa wakiegemea wapi? Walikuwa wakiegemea kwenye ukweli kwamba nchi hiyo *ilikuwa* ni mali yao. Hiyo ni kweli. Wakati Yoshua alipoigawanya nchi, Mungu aliwapa Israeli Ramoth-gileadi. Naye adui alikuwa amewasukuma nyuma kutoka kwenye nchi hiyo, nao walikuwa wakiikalia hiyo nchi wenyewe.

100 Sasa, angalieni, ndugu zangu wa Kipentekoste. Mnaona? Hiyo ni kweli, nchi hiyo ni mali yao, bali inaweza kuchukuliwa na adui na kukaliwa mpaka mambo yafanywe sawa. Rudini kwenye Neno. Hmm? Haidhuru tunadai nini, hatuna budi kurudi, na kuambatana na Neno, kwa kuwa hivyo ndivyo—hivyo ndivyo Mungu alivyolifanya. Hatuna budi kurudi kwenye ninii, kujiweka sawa na Neno. Kujiweka sawa na Mungu na Neno Lake, ndipo halina budi kutenda kazi.

101 Lakini manabii hawa walisema, "Kwea kule, Bwana yu pamoja nawe." Na mbona, mmoja wao, Zedekia pale, ninaamini, alikuwa amejitengenezea pembe mbili, naye akasema, "Utazichukua pembe hizi na—na kumsukuma adui moja kwa moja kutoka nchini."

102 Lakini mwajua, mtu halisi wa kiroho, natumaini nyumba nzima imejaa hao, usiku wa leo, mnaona, hilo halikusikika sawa kwa Yehoshafati, maana alikuwa ni mtu mzuri.

103 Mia nne, labda mara mbili ya tulio nao hapa usiku wa leo, wote wakitabiri kwa moyo mmoja. Akasema, "Sasa, hao hapo, hao hapo." Kasema, "Hiyo ndiyo ishara yetu."

104 Naye nabii huyu akasema, “Nitakufanyia ishara.” Akachukua pembe mbili, na kusema, “Chukua hizi, nawe utawasukumia mbali kabisa, hiyo ni ‘BWANA ASEMA HIVI.’”

105 Lakini Yehoshafati akasema, “Kuna kasoro fulani tu hapo, siwezi kulinyoshea kidole, lakini kuna kasoro.” Kasema, “Hivi huna mwingine?” Akasema, “Loo, naam, huenda tukamwita mwingine. Yeye ni mtakatifu anayejibingirisha hapa chini, jamaa mdogo anayeitwa Mikaya, ila namchukia. Mbona,” akasema, “yeye—yeye—yeye kila mara anatabiri mabaya dhidi yangu.”

“Loo,” akasema, “mfalme na asiseme hivyo, bali hebu tumsikie.”

106 Kwa hiyo wakawatuma wadhamini kule, halmashauri ya mashemasi, kasema, “Sasa, angalia, unajua, huenda ukafanywa mzee wa jimbo ama kitu fulani, kama utaungana tu nao sasa. Useme jambo lile lile wanalosema.”

Na, loo, ungeweza kuwazia ukimzungumzia mtu wa Mungu namna hiyo? Mikaya akasema, “Kama Bwana Mungu aishivyo, nitasema tu yale Yeye anayoniambia niseme.”

107 Haya basi, hao ndio aina wasimamao. Naam, bwana. Mnaona? Alikuwa nini? Alikuwa ni ishara. Alikuwa ni ishara papo hapo, jambo fulani litatukia, Mungu atatimiza Neno Lake, maana tayari alikuwa amemwambia nabii halisi wa Mungu, Eliya, yale yatakayowapata A—Ahabu na Yezebeli wote wawili kwa uovu wao. Naye anawezaje kubariki uovu ambao haujatubiwa?

108 Anawezaje kufanya mambo haya katika upotovu ambao kanisa linasimama ndani yake siku hizi, pamoja na tofauti zake, na ubinafsi, na—na kulikana Neno, na mifano ya utauwa, na kukana nguvu za Mungu za Neno Lake? Anawezaje kuweka baraka juu ya hilo? Hawezi kufanya hivyo. Hakika hatafanya. Huna budi kurudi kwenye jambo halisi, la kweli.

109 Na—naye akasema—akasema, “Nipe usiku wa leo.” Bwana akamtokea, nanyi mnajua huo unabii ulivyokuwa. Na kwa hiyo, ilikuwa ni kweli kabisa, ishara.

110 Sasa, sasa, kama kuna unabii wa kweli. . .Sasa, tunajifunza. . .Sasa, baada ya Andiko hilo, katika Mathayo 24, tunajua kuna kweli na uongo pia, tunajua hilo. Kila mnapoona ukweli, uongo upo pia, kumbukeni.

111 Ni nini—ni nini—uongo ni nini? Ni kweli iliyopotoshwa. Kwa kweli lilikuwa ni kweli, halafu mtu fulani akalinukuu vibaya, akalifanya uongo. Kitu kibaya ni nini? Ni kitu cha kweli kilichopotoshwa. Mnaona? Kila kitu, ibilisi hawezi kuumba chochote, na kila kitu cha uongo, ibilisi alipotosha kilichokuwa cha kweli akakifanya cha uongo. Na kama kuna Neno halisi la Mungu, kuna *linaloitwa* Neno la Mungu ambalo ni la uongo.

Hiyo ni kweli. Kama kuna nabii wa kweli, Mathayo 24, Yesu alisema, "Jihadharini na manabii wa uongo." Kwa hiyo kuna manabii wa uongo, kama vile kulivyo na manabii wa kweli, bali nabii wa kweli, jinsi utakavyomtambua, daima atadumu na Neno.

112 Hivyo ndivyo hasa Mikaya alivyofanya, alidumu kabisa na Neno la Bwana, maana Neno la Bwana, yeye alijua lilikuwa ni Neno, lilimjia nabii. Sasa, tunajisikia wa kidini. Mnaona? Mnaona? Neno la Bwana, linasimama haidhuru ni kitu gani kinachoendelea, Makanisa yanainuka, yanaanguka; watu wanainuka, wanaanguka; chochote kile, huinuka na kuanguka, bali Neno la Mungu halitaanguka kamwe, kwa kuwa ni Mungu. Ni Mungu katika maandishi. Kweli.

113 Hiyo ndiyo sababu una Uzima wa Milele, kila kitu kilichokuwa na mwanzo kina mwisho. Kama una mwanzo, una mwisho, hiyo ndiyo sababu mwili huu hauna budi kufa, ulikuwa na mwanzo. Lakini nafsi iliyo ndani yako, kama ni Mungu, Roho Mtakatifu, ndani yako, ni kitu gani? Ni wazo la Mungu lililokusudiwa. Neno ni nini? Ni wazo lililotamkwa. Mnaona? Naye Mungu, kabla hapajakuwapo na ulimwengu, alikuwazia. Amina. Aliliwazia Kanisa. Hakika. Unaona?

114 Halafu basi, unapozaliwa mara ya pili, Yesu alisema angempa Uzima wa Milele, nalo neno la Kiyunani, *Zoe*, ni "Uzima wa Mungu Mwenyewe." Wewe ni sehemu ya Mungu nawe hutaangamia kamwe, "Nitamfufua tena katika siku ya mwisho," hawezi kuangamia, kwa sababu ni wa Milele, hakuanza kamwe, hakuanza kamwe, kwa hiyo hawezi kwisha. Ulikuwa ni wazo la Mungu kabla Yeye hajakudhihirisha katika Neno, basi lilipofanyika Neno, ndipo likafanyika mwili.

115 Na hiyo ndiyo sababu haikumbidi Yesu kuomba. Sina budi kuomba, huna budi kuomba, kwa sababu tumepotoshwa kutokana na tendo la kujuana kimwili, tunapoletwa na baba na mama, kiumbe kipotovu. Hatuko katika asili, Mungu hapo mwanzo kamwe hakusema, "Ewe mwanamke, mzae mtu." Alimwumba mtu kwa Neno Lake, na kwa hiyo Yesu alikuwa ni Neno, mwanamume hakuhusika, wala mwanamke. La, bwana.

116 Yeye alikuwa, Yeye si chavua ya Mariamu, hilo linarusha wazo lako la Kikatoliki maili milioni moja. Hakuwa na uhusiano wowote na Mariamu, Mariamu alikuwa ni kiangulio tu, hivyo tu, Yeye hata hakumwita "Mama." Nionyeshe wakati mmoja Yeye alipomwita "Mama." Alisema, "Mwanamke." Amina. Hivyo tu ndivyo alivyokuwa, mwanamke ambaye Mungu alimtumia, hiyo ni kweli, si mungu mke. Ati "Mama wa Mungu," ni jambo la kipumbavu jinsi gani! Ati Mama wa Mungu? Ni nani anayeweza kutoa, kumfanya Mungu kuwa na mama? Basi mama wa mama wa Mungu alikuwa ni nani? Loo, jamani!

117 Mnanena kuhusu "Uwana wa Milele." Mwana ana mwanzo, Milele haiwezi kuanza, haiwezi kuanza. Na hapo . . . Daima imekuwapo. Anawezaje kuwa Mwana wa Milele? Loo, jamani. Unafanyaje . . . ? Mimi ni mjinga, na ninajua vizuri zaidi kuliko hivyo. Hakika.

118 Yeye alikuwa Chapa ya Mungu iliyodhihirishwa, maana Yeye alikuwa ni wazo la Mungu lililodhihirishwa na Neno Lake. Mungu alisema, "Na iwe," ikawa. Alimtia Mariamu uvuli. Alimnyonyesha, kweli, bila shaka. Unafanya jambo lile lile usiku wa leo, unapomlisha sifa na utukufu wako, kweli, kufanya ushirika pamoja na Mungu.

119 Sasa, angalia, Yeye alikuwa ni Neno. Unaona sasa, Yesu, Yeye alisema hivi tu kwa sababu Yeye alikuwa ni Neno, bali kwetu sisi, hatuna budi kumwendea Mungu kwa Neno. Unaona? Neno huwajia manabii, wao si Neno. Katika Agano la Kale, sasa, Eliya, Musa, hao manabii wote wakuu, hawakuwa ni Neno, walikuwa, uh, walikuwa ni mwili uliopotoshwa na . . . uliojiliwa na Neno la Mungu. Biblia ilisema Neno la Mungu liliwajia manabii. Hawakuwa ni Neno, bali Yesu alikuwa ni Neno. Amina. Amina. Loo, ninapenda tu hilo! Vema.

120 Sasa, kwa nini Yeye kamwe hakushindwa kudumu moja kwa moja na Neno hilo? Shetani alijaribu kulipotosha kama alivyofanya kwa Hawa, Yeye akasema, "Imeandikwa utaninii . . . Alikuwa amemwagizia Malaika, asije akajikwaa mguu katika jiwe."

121 Akasema, "Pia imeandikwa." Unaona? Loo, Yeye alilisukumia tu kwake moja kwa moja. Ndipo akasema, "Mtu hataishi kwa mkate pekee, bali kwa kila," *kila*, si kidogo hapa, na kidogo pale, na kulichanganya na baadhi ya theolojia ya kujibunia ya watu wa kilimwengu, wenye nia za kibinadamu, "bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu, mtu ataishi kwa Hilo." Kila Neno, kila Neno! Kila Neno la Mungu, watu wataishi kwalo, Hilo ndilo atakaloishia. Yesu alisema hivyo, Naye alikuwa ni Neno.

122 Kwa hiyo sasa, basi kama nabii wa kweli akidumu na Neno, nawe unaona dhihirisho la Neno, kama vile Mikaya alivyofanya, kama Musa, kama wote walivyofanya, basi nabii wa uongo angekuwa ni mtu ambaye angekufanya wewe, angejaribu kukufanya ufadhaike kuhusu ishara za Neno la Mungu, angekuwa ni nabii wa uongo. Yesu alisema ujihadhari nao, nao watawapumbaza ama kuwapoteza walio Wateule kama yamkini. Mnaona, watakuja moja kwa moja kule juu, na kudai kuwa ni kila kitu kingine, bali wao kamwe hawaninii . . . wanapoanza kuondoka kwenye Neno hilo, wewe ondoka pia, waondokee, dumu na Neno.

123 Tunafikia majira ninayowazia sasa, watayaita "Kwaresima." Kwaresima, kitu gani? Nafikiri hivyo ndivyo mnavyoyaita, kitu

kama hicho. Hilo ni sawa. Wakitaka, ni—nitaambatana nao umbali *huo*, lakini, mwajua, hawanywi pombe, wala hawavuti sigara, wala hawafanyi *hiki-na-hiki*, Waprotestanti, Wakatoliki, na wote, hilo ni sawa, wala siamini katika kufanya hivyo, hakika, niliacha hayo, lakini baada ya siku arobaini, ndipo mnaniacha tena.

124 Nitaambatana nanyi umbali *huo*, kisha mnarudi matopeni tena, sitaki kurudi nyuma, hebu tuendelee kusonga mbele. Kama ni siku arobaini nzuri, hebu na tuendelee, na kuendelea, na kuendelea. Mnaona? Dumu na Neno, dumu na Uzima wa Milele, dumu na Kristo. Kama likifanya vizuri kwa siku arobaini, litafanya kazi maishani mwako mwote. Hakika, kwa sababu Neno ni la Milele. Vema.

125 Manabii wa uongo, ama makafiri wasioamini, lolote unalotaka kuwaita, maana mtu yeyote asiyeamini Neno ni kafiri, hiyo ni kweli kabisa, nao wame—wamefadhaika, nao—nao wanashuhudia Neno uongo, wanasema, "Neno halimaanishi *hivi*." Linamaanisha vile hasa linavyosema.

126 Wanasema, "Vema, hiyo ilikuwa ni kwa ajili ya mitume, hiyo ilikuwa ni kwa ajili ya . . . " Vema, wanawezaje kumhubiri Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele, basi? Unaona? Neno linasema Yeye ni yule yule jana. "Vema, kwa njia fulani Yeye ni yule yule." Yeye ni yule yule kwa kila njia. Naam, bwana. Naam, hakika ndivyo alivyo.

127 Hebu tuone, naam, bwana, manabii wa uongo, ama wapagani wasioamini, hufanya ishara za uongo. Wangekuwa na ishara ya namna gani basi? Sasa, mnakumbuka, wanaenda kwa wote . . . Hao si—hao si wakomunisti, hao ni wa kidini. Mkomunisti, kamwe hampumbazi mtu yeyote. Hakika. Lakini watu wa aina hii watawapoteza walio Wateule kama yamkini. Mnaona? Atasema nini? Sio, "Njoo uzaliwe," bali, "Njoo *ukajiunge*." Um-hum. Huyo ni nabii wa uongo. Mnaona? "Njoo ukajiunge tena." Lakini hupaswi kuunganishwa tena, bali kuzaliwa mara ya pili.

128 Ishara za uongo, um-hum, pia wanasema, sasa, kwa watu, "Msiamini ishara hizo." Bila shaka, wanafadhaishwa nazo, hivyo ndivyo Biblia ilivyosema wangekuwa. Mnaona? Wangefadhaishwa na ishara za Mungu, ishara za Mbinguni.

129 Mungu angeshusha ishara kutoka Mbinguni za Neno Lake, nao watu, wapagani, vema, walisema, "Usichukue elimu yao, kaa mbali na elimu yao." Sasa, wame—wame—wameelimika, usijifunze njia zao. Wana njia za seminari, na kila namna za njia kama hizo, kaa mbali nao, wewe dumu moja kwa moja na Neno. Unaona? Wewe kaa mbali nao kabisa, maana watakuwa na ishara ya uongo.

130 Kwa kuwa Yesu alisema katika—katika Marko mlango wa 16, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Naam, bwana.

Hiyo ni kweli. Kwa hiyo kama ishara hizo hazifuati, naye anasema, “Loo, hizo hazihitajiki siku hizi,” o—ondoka tu. Mbona, ninii tu—kama tu, loo, jamani, kaa mbali nao, kama mtoto aliyeungua karibu na jiko, jiepushe tu nao, huko nyuma kabisa. Unaona? Ondokeni moja kwa moja kwake. Akiwaambia watu, “Msiamini ishara hizi.” [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Nao wanawezaje kufanya hivyo? Ingawa ishara hiyo ni ishara ya kweli ya Neno iliyotumwa na Mungu kwa ajili ya siku ile hasa wanayoishi!

131 Sasa, nilimtaja Mikaya muda mfupi uliopita, hebu turudi tu nyuma. Nitachukua baadhi ya manabii hao katika dakika chache, Bwana akipenda, lakini nitarudi tu kwa Mikaya. Sasa, angalieni, kwa nini hao wahubiri kule chini hawakuweza kuona ya kwamba Neno la Bwana lilikuwa limemlaani Ahabu, likamlaani Yezebeli, na laana ilikuwa juu ya nchi? Basi angewezaje kuibariki wakati laana ilikuwa juu yake? Mnaona, asingeweza kufanya hivyo. Mungu hafanyi mambo kama hayo. Mnaona?

132 Na hapa Mikaya, na mtu huyo amesimama pale chini ya uvuvio, sawasawa kabisa na Neno, vile hasa Neno la Mungu lilivyosema, kwa kuwa Neno la Mungu lilisema ya kwamba mbwa watairamba damu ya Ahabu kisha wangemla Yezebeli. Neno la Bwana lililonenwa na nabii lilisema hivyo, na Hilo lilikuwa ni Neno la Bwana kwa sababu lilimjia nabii.

133 Na huyu hapa nabii mwingine akikaa moja kwa moja pamoja na Neno, ilionekana kana kwamba Ahabu angeona hilo. Ilionekana kana kwamba wangelitambua hilo. Mnaona? Ndipo akageuka na kumlaani maskini jamaa huyo, ndipo huyo—huyo askofu akamwendea na kumpiga kofi usoni. Wala mtu huyo hakufanya hivyo kinafiki, aliamini alikuwa sahihi.

134 “Unawezaje kujua, Ndugu Branham, mema au mabaya?” Yapime kwa Neno. Hilo litaonyesha kama wako sahihi ama si sahihi, dumu moja kwa moja na hilo Neno, uone kinachotukia. Unaona? Litupe tu Neno pale chini uone mahali walipo. “Loo, vema, unaona kwamba . . . ” Loo, basi nenda tu mara moja papo hapo. Unaona? Naam. Dumu tu moja kwa moja na hilo Neno.

135 Kwa hiyo, vema, kama walikuwa wamempa Mikaya jaribio la Neno, yeye alithibitisha kwamba alikuwa nalo asilimia mia moja. Sasa, wanasema, “Ngoja kidogo,” unaona, “Mungu alitupa sisi.” Hiyo ni kweli.

136 Mungu alitupa ahadi ya Roho Mtakatifu. Petro alisema kwenye Siku ya Pentekoste, mwajua, “Tubuni kila mmoja wenu, mkabatizwe, katika Jina la Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi, mtapokea Kipawa cha Roho Mtakatifu. Ahadi hii ni kwa kila kizazi.” Mnaona? Hao ni sisi. Hiyo inamaanisha sisi, bali ni masharti. Kamwe huwezi kuipata kwa njia yoyote, huna budi kufuata maagizo. Hiyo ni kweli kabisa.

137 Nchi hiyo kweli ilikuwa mali yao, bali iliwabidi kufuata maagizo. Nayo maagizo ya Bwana hayakuwa ni kumpa Ahabu, alilaaniwa. Na chochote ambacho Mungu analaani na kuthibitisha hayuko pamoja nacho, kiondokee. Amina. Hiyo ilikuwa ni bunduki yenye mitutu miwili, sivyo? Naam, bwana. Kama Mungu amethibitisha Yeye hayuko pamoja na kitu hicho, usikikaribie, hiyo ni kweli, kwanza kabisa hakina faida. Mungu amekihukumu, nami nina hakika sitaki kukikaribia, naam, bwana, nina matatizo chungu nzima jinsi kilivyo, badala ya kuingia katika kitu kama *hicho*.

138 Sasa, yeye alisema. . .Sasa, tunataka kukaa hili. . .Jamaa hawa walimchukua maskini mhubiri huyo na kusema, "Mweke kwenye vyumba vya ndani, huko nyuma kabisa, na kumfungia, moja ya hizi kozi kubwa hapa za mbao, na kumfunga gerezani, na—na kumlisha tu mkate na maji mpaka nitakaporudi kwa amani, ndipo nitamshughulikia jamaa huyu, mwana wa Imla."

139 Akasema, "Ukirudi kamwe, basi Bwana hajasema nami." Hakulegea, maana alijua unabii wake. Roho, li—li—lile ono lililomjia lililingana kabisa na Neno. Haya basi. Sasa, mnaona ninachofikia? Kama ninii yako—kama ono lako haliambatani kabisa na Neno, afadhali uachane nalo. Haidhuru unajaribu kudai ahadi ya namna gani, afadhali urudi sawasawa na Neno. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli kabisa. Unaona?

140 Ingawa ni ishara ya kweli ya Mungu kwa ajili ya siku hii, iliyonenwa katika Neno, Mungu alisema jambo hilo lingetukia wakati huo tu, wangali watalikana, waseme, "Hakuna kitu kwake," hiyo ni kweli, "usiamini jambo hilo." Loo, jamani.

141 Kwa Neno Lake la kweli la kinabii, Yeye daima ametoa ishara za Kimaandiko kabla hajatuma hukumu, mnaona, kwa Neno Lake. Yeye atalinena huko nyuma kabisa, kisha litalifikia Neno, na hapa atakuja mmoja wa watumishi Wake akitangaza Neno hilo, jinsi tu lilivyo. Mnaona? Naye daima hufanya hivyo kabla hajatuma hukumu aliyoahidi. Yeye daima. . . Ndipo mtu fulani anakuja na ukweli wa Kimaandiko na Mungu akishuhudia, Waebrania 2:4 ilisema hivyo, "Akishuhudia kwa ishara na maajabu Yake, Mungu akilithibitisha Neno," Marko 16, "kwa ishara na maajabu." Mungu akithibitisha yale yaliyohubiriwa. Mnaona?

142 Hakika, huenda ulikuwa na ibada ndogo ya uponyaji, ambayo huenda ikafanya kazi vizuri, lakini vipi kuhusu mengine yote? Mnaona? Unaweza kulichukua Neno na kulifanya litende kazi papa *hapa*, kisha uchukue yaliyosalia, Nalo litafanya kazi mahali Pake, vivyo hivyo kabisa, kila mahali. Kila mahali unapoliweka Neno, litafanya kazi kama liko katika njia sahihi, imani nyuma Yake kuliamini, basi halina budi kukua.

143 Niliona hivi majuzi ambapo walichukua mbegu ya alizeti, naamini ndiyo, ama labda ilikuwa ni ngano, kutoka kwenye

maghala ya Misri, ambako Yusufu alikuwa ameziweka huko nyuma, yapata miaka elfu mbili mia nane iliyopita, wakaipanda, ikafanya zao la ngano. Haidhuru ilikuwa na umri gani, ingali ilikuwa na uhai ndani yake, kwa sababu ilikuwa ni mbegu iliyorutubishwa. Haidhuru ahadi hizo zimetolewa kwa muda gani, ni kwa ajili yenu na kwa watoto wenu, na kwa wale walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie. Huna budi kuichukua mbegu hiyo na maji, amina, na chochote hiyo mbegu ilicho kitazaa mazao yaliyo mbegu hiyo.

144 Tumekuwa na uamsho mkuu, hapana shaka, bali umekuwa ni uamsho wa kimadhehebu. Kwa nini? Kwa sababu tumepanda mbegu za kimadhehebu. Kweli. Wakati Roho Mtakatifu anaposhuka, kama tu mvua juu ya wenye haki na wasio haki, mvua inanyesha, inafanya gugu likue na kuifanya ngano ikue pia, yote miwili inafurahi tu kama huo mwingine, bali matunda yao mnayajua. Tunajaribu kufanya nini? "Milioni moja zaidi," na shirika *hili* likilishinda *lile*, dhehebu *hili* likilishinda *lile*.

145 Tumekuwa na Billy Graham, ndio kwanza wawe na uamsho, kwa Wabaptisti, mmoja wa wavulana wenu hapa, mtu mashuhuri wa Mungu, pia. Naam. Wapentekoste walikuwa na uamsho, Oral Roberts. Loo, jamani, wengi wao, uamsho mkuu. Jamani, waliongezeka kwa idadi hata wasivyotarajia. Imekuwaje, sasa imekwisha?

146 Hivi mlijua Yoeli alisema kutakuwako na mvua ya masika na mvua ya vuli? *Mvua ya masika*, m-a-s-i-k-a, linamaanisha "moureh," neno la Kiebrania, ambalo linamaanisha "mvua ya kupanda," kupanda mazao. Hiyo ndiyo sababu. . .Mlivuna nini? Loo, madhehebu yameundwa, lakini Mungu yuko wapi? Mlipanda mbegu za kimadhehebu, wakati Roho Mtakatifu aliposhuka, uamsho wa kimadhehebu ulifanyika.

147 Tunachohitaji ni, "Rudini kwenye Neno!" Rudini kwenye Neno halisi la Mungu, na mumzalie Kristo na Neno Bibi-arusi. Hiyo ni kweli, kurudi kwenye Neno.

148 Acha dhehebu, hilo ni sawa, sina kitu dhidi yake, lakini kila mtu hana budi kupiga ngumi chache, mwajua, kwa sababu wasipofanya hivyo, wanatolewa nje. Mungu aturehemu, kupiga ngumi. Sema ukweli, la sivyo nyamaza. Um-hum. Hiyo ni kweli. Liseme tu jinsi lilivyoandikwa, uone kama Mungu halithibitishi. Ninawapa changamoto kuliamini, ninajua ni kweli. Mnaona?

149 Lakini huna budi kudumu moja kwa moja na Neno na kuliamini, si kujipenyeza tu *huku* na *huko*, na kusema, "Nitadonoa na kujaribu." Hufanyi hivyo. La, la, huna budi kuja kwa moyo wote, "Ni Neno Lako, Bwana, ninaliamini." Mungu atalifanya. . .Litaanza kutenda kazi papo hapo. Naam, bwana.

150 Naam, bwana, Yeye daima ametuma, kabla ya hukumu Zake, mtu mwenye Neno la Kimaandiko, akionyesha ishara za

Kimaandiko kabla hajalituma. Naye asiyeamini analikosa Hilo maili milioni moja. Kwa nini? Amefadhaishwa Nalo, amevunjika moyo. Kwa nini? Kwa sababu yeye haliamini. Amina. Lakini daima huleta mavuno Yake vivyo hivyo.

151 Mnaona, asiyeamini, "Loo," anasema, "upuuzi mtupu, *tsk*, *tsk*, *tsk*, *tsk*, *tsk*, upuuzi mtupu, loo, jamani, hakuna chochote hapo. Mbona, unajua siku za miujiza zimepita, hakuna kitu kama hicho. Loo, jamani, hilo ni baya sana, lundo tu la takataka, hakuna lingine." Lakini wanaendelea vivyo hivyo.

152 Vema, ungeweza kuwazia Moabu kusimama pale akimwangalia Israeli, ndugu yake? Hata hivyo, alisimama. Hivi mlijua yule nabii wa uongo kule juu, alitoa masharti ya aina ile ile ya ki—kitheolojia ambayo Musa alikuwa akitoa, huko chini katika kambi nyingine? Hiyo ni kweli. Huyu hapa Balaamu akaja, Askofu Balaamu, akaja huko katika nchi hiyo kubwa taratibu ya Moabu. Binti wa Lutu, huko ndiko lilikotoka. Si Mungu mwingine, Mungu yule yule. Akapanda kule na kuweka madhabahu saba. Yehova alihitaji nini? Nambari kamilifu, Yehova. Dhabihu saba, dhabihu safi, jinsi Yehova alivyo hasa, hiyo ndiyo Musa aliyokuwa nayo hapa chini, ile ile hasa. Kondoo dume saba, wakinena juu ya kuja kwa Mwana wa Mungu, kondoo dume saba. Naam, bwana. Lakini, loo, ndugu, alikosa kuona ule Mwamba uliopigwa, yule nyoka wa shaba.

153 Hilo ndilo alilokosa kuona, na ni jambo lile lile siku hizi. Wanakosa kumwona huyo Roho Mtakatifu akitenda kazi katika Neno na ahadi ya Mungu, akileta ishara na maajabu aliyoahidi. Hawakuamini jambo hilo, hiyo ndiyo sababu.

154 Sasa, hebu na tuchukue wachache tu, kwa muda kidogo tu sasa, dakika zingine chache. Nuhu na ishara zake alizopewa na Mungu, mnaamini alikuwa na ishara aliyopewa na Mungu? Hakika, alikuwa nayo. Alitumwa na Mungu, nabii wa Mungu aliyetabiri, na kuonyesha ishara kuu na maajabu, kwamba kutakuwako na ishara kuu mbinguni: Mawingu yangetanda, mvua ingenyesha. Kamwe mvua haikunyesha katika siku hizo, ishara yake aliyopewa na Mungu. Alisimama moja kwa moja kwenye mlango wake wa safina na kuhubiri miaka mia moja na ishirini, nao wakamcheka na kumdhihaki.

155 Mnajua Yesu alirejelea kwenye hilo, Mathayo, mlango wa 24, tena, kuhusu siku za Nuhu? "Katika siku za Nuhu . . . " Alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, walikuwa wakila, wakinywa, wakioa, wakiolewa." Alisema jambo lile lile katika Mathayo 24 hapa, hiyo ni kweli kabisa, kasema wangefanya jambo lile lile. Na hivi mliona moja kwa moja hapo chini Yeye alisema, pia, "Pia kutakuwa na mambo ya kutisha mbinguni, ishara mbinguni na duniani." Hiyo ni kweli? Sasa, nini—nini, Yeremia alisema nini hapa? "Msifadhaike kwa ajili ya ishara mbinguni."

156 Angalieni hapa, mnasema, "Ati ishara mbinguni?" Mbona, wameshangaa, hata Pentagon, mliiona si muda mrefu uliopita, swala hili lote hapa la kisahani kirukacho, walishangaa kilikuwa ni kitu gani. Hawawezi kukielezea bado, karibu ni nguvu zisizoonekana, zinazoshuka kule, na hata hivyo ki—ki—kina akili, kitaninii. . . Sasa, mimi si mtu wa kisahani kirukacho, upuuzi huu wote hapa unaosimuliwa juu yake, huo, huo si kitu kwa hicho, usiamini huo. Lakini ni ishara, hasa. Ni kwa nini vinaning'inia moja kwa moja juu ya Pentagon? Ni kwa nini viko moja kwa moja huko Washington, ambako vinaonekana wakati wote, sikuzote, hata vingali? Tutalifikia hilo baada ya kitambo kidogo, tuone kama Yeye hakusema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu." Hiyo ni kweli.

157 Musa na ishara yake, ishara aliyopewa na Mungu, ishara ya Kimaandiko, je, mnaamini ishara ya Musa ilikuwa ya Kimaandiko? Musa alijuaje? Musa alijuaje ilikuwa ni Mungu? Aliposhuka kwenda kule alielewa, akiwa amezaliwa kuwa nabii, alikuwa na Neno la Bwana alilolijua, kwa hiyo anashuka huko chini kuwakomboa Israeli, naye akakuta kwamba alikuwa nje ya wakati, hao watu hawakumtaka.

158 Nabii hawezi kamwe kutoa Ujumbe wake isipokuwa watu wawe wanataka kuusikia, kwa hiyo Mungu akamwita tu nabii Wake nyikani. Hakika. Akampeleka huko nje na kuwaacha watu wateseke zaidi kidogo, mpaka walipokuwa tayari. Musa alikuwa tayari, Mungu alikuwa tayari, bali hao watu hawakuwa tayari, walikaa miaka arobaini zaidi kwa sababu hawakuwa tayari, hiyo ni kweli kabisa.

159 Lakini wakati Musa alipokiona hiki kichaka kilichowaka moto, alikuwa ameona moto mwingi, nadhani, lakini wakati Sauti hii ilipotoka kwenye kile kichaka, huenda, huenda alikuwa amesikia sauti nyingi sana, lakini wakati Sauti hii ilipotoka kwenye hicho kichaka, mnajua kile ilichosema? Ilimnukulia Maandiko. Na halafu ilikuwa ni ishara ya Kimaandiko, kwa sababu Mungu alimwambia Ibrahimu ya kwamba watu Wake wangekuwa, wangekuwa wageni katika nchi ya kigeni kwa muda wa miaka mia nne, ndipo Yeye angewakomboa kwa mkono wenye nguvu na uweza.

160 Mu-. . . Yeye alisema, "Niko tayari kutimiza hilo, Musa, ninakutuma huko." Amina. "Ninataka kufanya Maandiko. . . Nitakupa Maandiko. Chukua maskini fimbo hii uliyo nayo mkononi mwako sasa, uende Misri upesi uwezavyo." Unaona? Kwa kuwa alikuwa anaenda kufanya Neno Lake kutimia.

161 Mnajua walichofanya huko chini? Wamisri ndio waliosema, "Musa, loo, nabii mkuu wa Bwana." Wakamcheka, nao wakafadhaishwa na ishara alizofanya. Hiyo ni kweli?

162 Mbona, hata Israeli walifadhaika pamoja naye, kwa ishara alizokuwa akifanya . . . "Kwa nini . . .? Mbona, una—unatufanya tufanye kazi ngumu sana, mbona, angalia hapa, mikono yetu, inatubidi kutengeneza makapi, na kadhalika," huku Musa akifanya ishara zile zile alizopewa na Mungu, nao wangali hawakuweza kuelewa jambo hilo. Hiyo ni kweli kabisa. Mnaona? Musa aliwapa ishara, ikavunja Misri moyo, ikasumbua . . . kwa ishara za Mungu, kwa ishara zilizotabiriwa.

163 Mungu alimwambia Ibrahimu, baba wa ile ahadi, ya kwamba uzao wake, Israeli, wangekuwa wageni katika nchi ya ugeni, Naye angeonyesha mkono Wake wenye nguvu kwa kuwakomboa. Na hapa alikuwapo huyo mtu, kulingana na Maandiko, huyo hapo mtu mwenye ishara zilizoahidiwa, nao hawakuamini, wakaangamia, bila shaka.

164 Ungeweza kuwazia juu ya Ezekieli, nabii mwingine? Mbona, Ezekieli, mtu huyo, Mungu alimwambia, "Nitaninii . . . " Kabla tu ya hukumu kuja, Mungu alimtuma Musa kabla ya hukumu, akamtuma Nuhu kabla ya hukumu, alimtuma Nuhu na kuwachukua watu wote, ninamaanisha, Musa, akawaleta watu katika—katika—katika nchi ya . . . ambapo wao, na, ambapo wasingesumbuliwa na yale mapigo. Naye akamtuma Nuhu, na kuwaingiza waaminio wote ndani ya safina, na kuwaangamiza wasioamini wake, wa ishara ya Nuhu, akijenga safina, akiandaa, akitabiri yale yatakayotukia. Wote walioingia safinani waliokolewa; wote walioingia Gosheni waliokolewa.

165 Na huyu hapa Ezekieli anakuja kabla tu ya Mungu kuwapeleka Babeli. Akasema, "Nenda ulale kwa ubavu wako wa kushoto kwa muda wa siku mia tatu na tisini." Kasema, "Nimekuwekea mzigo juu yako." Basi mngeweza kumwazia maskini nabii huyu mzee mwenye mvi akilala kwa ubavu kwenye malango ya—ya Yerusalemu katika Israeli? Basi watu wote waliopitia pale, walisema, "Mwangalieni mlokole yule, amelala pale, pamoja na maskini kitoweo mlichokiona huko juu, cha—cha—cha maharagwe na kadhalika," na kimechachuka kwa majuma kadhaa.

166 Naye huyo hapo amelala pale, naye akalala kwa ubavu wake wa kushoto kwa muda wa siku mia tatu na tisini, kisha Mungu akasema, "Geuka upande wako wa kuume ukalale arobaini zaidi." Mbona, ilikuwa ni fedheha.

167 Loo, Israeli walikuwa na *majivuno* kwelikweli, mwajua, jamani, wangeshirikiana na nchi nzima. Walitaka kuondolea mbali vitu kama manabii, bali walisahau ya kwamba Neno la Mungu liliwajia manabii. Walitaka kuchukua miungu yao, walitaka kuchukua njia yao waliyotaka kuliaminia.

168 Lakini Mungu alikuwa amewatumia nabii kwa ajili ya ishara, naye akafanya ishara, nao wakaipuuza ile ishara, nao wakaingia hukumuni. Muda gani? Kwa miaka mia nne

na thelathini, Yeye aliruhusu siku moja kwa mwaka mmoja kwao. Walipomcheka, kila siku waliyocheka ilimaanisha mwaka mwingine kifungoni. Naye akawapa ishara, wasingeiamini, la. Lakini Yeye aliwapeleka huko Babeli katika hukumu.

169 Loo, jamani, hebu tumwazie mwingine. Asubuhi moja ya kiangazi yenye joto, akishuka kwenye barabara ya Samaria, uso wake umejaa makunyanzi, maskini macho yake madogo yakiangalia juu angani, fimbo mkononi mwake, miguu yake mitupu imekanyaga chini, amejizungushia maskini kipande cha ngozi ya kondoo, alionekana kama mdudu aliyejaa manyoya akitoka pale, na kichwa chake chenye upara kikiangaza, fimbo mkononi mwake, ndugu, hatua zake zilikuwa tu kama kijana mwanamume akishuka barabarani, barabara ya Samaria.

170 Hakusitasita alipofika mbele ya Ahabu. Alikuwa amewahubiria muda mrefu kuhusu njia yao iliyolaaniwa, walikuwa na huu, labda, mkato wa nywele kichwa-maji katika siku hizo, wakimwiga mama taifa, mwajua. Alikuwa amechoka na Yezebeli na madoido yake yote. Loo, jinsi alivyowakemea! Mungu alimthibitisha kuonyesha ya kwamba alikuwa ni nabii wa Mungu. Naam, bwana. Lakini walitaka kuwa kama yule mama taifa, mwajua. Inajirudia mara nyingi sana, mwajua.

171 Taifa hili linafanana sana na Israeli. Mungu aliwapa nchi, wakaja na kuwafukuza wakaaji. Na kwa mara ya kwanza, walikuwa na Sulemani, walikuwa na Daudi, wafalme wazuri, ndipo Ahabu akaingia, mtu asiye na msimamo, sijui, kibaraka, hiyo ni kweli, huku Yezebeli, shingo ya ufalme, akimwongoza.

172 Nasi tulifanya jambo lile lile, tukaja na kuwafukuza Waisraeli, ama, kuwafukuza wale, sio...um...wahindi, tukawasukuma nje na kuwaua kwa njaa, hiyo ni kweli, tukaichukua nchi yao. Tulikuwa na Washington na Lincoln, lakini, ah! Nashangaa sasa! Tuna kitu fulani huko juu sasa pamoja na mfumo wa kale wa Yezebeli nyuma yake. Kama tu walichokuwa nacho hasa. Mungu atatutumia, Yeye aliahidi katika siku za mwisho, kulingana na Malaki 4, angemwinua mtu fulani, hiyo ni kweli, asingeachilia. Hiyo ni kweli.

173 Naye akiisha kufanya ishara zake zote na maajabu, ndugu, ninamaanisha, alikuwa na BWANA ASEMA HIVI, akashuka moja kwa moja kwenye makao makuu, na kusema, "Ninii...Hata umande hautaanguka kutoka mbinguni, mpaka nitakapouagiza," akaondoka moja kwa moja kwa kishindo. Kwa nini? Alikuwa na BWANA ASEMA HIVI. Ilikuwa—ilikuwa ni ishara, kulikuwa na ukame, mauti ilikuwa nchini.

174 Nafikiri wakati huu itakuwa ni mauti ya kiroho kwa baadhi ya watoto wa Yezebeli. Naam, bwana, mauti ya kiroho, unakauka. Ningeweza kusema jambo fulani, lakini afadhali niliache, maana ninaamini kuna kinasasauti huko nje kinachocheza huu. Sasa, loo, jamani, siku tunayoishi!

175 Naam, bwana. Baada ya huduma yake aliyopewa na Mungu, Neno la kweli la Mungu pamoja na ishara za kweli za maajabu yakiisha kukataliwa, mtu huyo angeweza kufanya nini? Aliwakemea kabisa. Yezebeli alimchukia, na mama taifa wake wote wa kisasa walimchukia. Hawakumpenda, la hasha. Walidhani alikuwa ni kitu cha kuchukiza, bali a—alikuwa mchungaji wake vivyo hivyo, loo, naam, Mchungaji Eliya. Loo, asingemdai, bali alikuwa ni mchungaji aliyetumwa na Mungu, alikuwa mchungaji wa Mungu kwake, hakumhurumia, alilimwaga Neno.

176 Nao wakamkataa, nao wakadhani alikuwa ni mjinga, ndipo—ndipo wakamfukuza. Hakuna hata moja ya madhehebu lingemtaka, walimfukuza, hilo halikulikomesha Neno, liliendelea tu vivyo hivyo. Kwa hiyo huko juu kabisa alingojea mpaka akawa na BWANA ASEMA HIVI kwa ajili ya Ahabu, naye akaja akamwambia. Ndipo alipofanya hivyo, njaa ikaipiga nchi. Hiyo ni kweli. Mnajua yaliyotukia, hakika. Huyo alikuwa ni Eliya kabla ya ukame.

177 Ninapenda kuona mmoja aliyemfananisha, mmoja alikuwa ni mfano wake, ama mfano wake halisi, wakati Yohana alipokuja kutimiza Ujumbe wa nabii wa mwisho, Malaki 3. Mwajua, Yohana alikuwa kwa namna fulani mvulana aliyezaliwa kigeni, mnajua hilo. Gabrieli alikuwa amemtokea mama yake, akamwambia yale angefanya, naye angekuwa mkuu, naye angewaita watoto wairudie imani ya baba zao, na kadhalika, na yote aliyokuwa anaenda kufanya. Malaki 3, "Ninamtuma mjumbe Wangu mbele ya uso Wangu." Na badala ya kwenda pamoja na baba yake kule chini kwenye shule ya baba huyu, aliondoka kwenda nyikani na akajiweka tayari.

178 Mwangalieni, ni kama tu Eliya: Aliishi mwituni kama Eliya, aliwachukia wanawake watovu wa uadilifu kama tu Eliya. Akamwambia maskini Herode, "Si halali kwako kumchukua," mke wa ndugu yake Filipo. Ilimgharimu kichwa chake, bali aliendelea tu vivyo hivyo, mnaona. Hakika. Alikuwa ni ishara.

179 Alikuwa akisema nini? "Nitawabatiza kwa maji kwa ajili ya toba, lakini anakuja Mmoja, tayari amesimama miongoni mwenu. Simjui, sijaiona ishara bado, lakini Yeye yuko miongoni mwenu." Alijua ya kwamba wakati huo ulikuwa umekaribia sana hata ilimbidi kuwa duniani wakati huo. Amina. "Kuna Mtu aliyesimama miongoni mwenu sasa hivi," akasema, "Msiyemjua. Lakini Yeye Ndiye, mimi sistahili kufungua viatu Vyake, bali Yeye atawabatiza kwa Roho Mtakatifu na kwa Moto, na pepeto Lake liko mkononi Mwake." Kasema, "Yeye atakuja moja ya siku hizi." Naam, bwana.

180 Siku moja Yesu alikuja akitembea, ndipo Yohana akaangalia juu, akasema, "Huyo hapo, Huyo hapo Mwana-kondoo wa Mungu Aichukuaye dhambi ya ulimwengu." Yesu, alipokuja

duniani, alifanya yale hasa Neno lilisema angefanya kwa ajili ya ishara kwa Israeli, kabla hawajahamishwa, na ndio kwanza sasa hivi wanarudi kwa ajili ya . . . tangu miaka elfu mbili iliyopita, tangu walipomkataa.

181 Israeli wataongoka wote kwa wakati mmoja, bila shaka wao ni—wao ni watu, wao ni taifa, Mungu huwashughulikia Israeli kama taifa, bali watu kutoka kwa Mataifa kama Bibi-arusi Wake. Israeli ni taifa, sasa hivi wanarudi kwenye nchi ya wenyeji wao, ishara kuu. Natumaini tunaweza kulifikia katika ninii, dakika chache tu. Lakini sina ila kama dakika tano ama kumi zilizosalia, nasi tutapanga mstari wa maombi, tutakapofika hapa chini ambapo ninataka kusema yale ninayotaka kusema, usiku wa leo. Mnaona? Huu ni msingi mkubwa mno, bali utasimama.

182 Yesu alishuhudia Neno. Yeye alikuwa ni Masihi, Mtiwa Mafuta. *Kristo* maana yake ni "Aliyetiwa Mafuta, yule Masihi, Yule aliyetumwa, Aliyetiwa Mafuta, Mtu aliyetiwa mafuta kwa Neno la Mungu na Roho wa Mungu." Yeye alikuwa ni Neno, alikuwa Neno lililotiwa mafuta. Amina. Yeye alishuhudia jambo hilo, yale hasa Musa nyuma hapa katika Kumbukumbu la Torati alisema Yeye—Yeye angefanya, alisema, "Bwana Mungu Wako atakuondokeshea Nabii, aliye kama Mimi." Angekuwa ni Nabii.

183 Na wakati, Simoni Petro alipojua jambo hili, na aliposikia . . . Ndugu yake, Andrea, alikesha usiku kucha pamoja Naye. Mwajua, hiyo ni njia nzuri ya kufanya, kukaa usiku kucha pamoja Naye. Um-hum. Mtu fulani hawezi kukaa pamoja Naye dakika tano, lakini Andrea alikaa usiku kucha, ndipo basi angeweza kweli kumwambia ndugu yake, "Hebu tushuke twende tukajaribu tena." La. "Tutaonana usiku wa leo." La. Akasema, "Njoo pamoja nami, uone Yule niliyemwona." Alijua alikuwa amempata, alikuwa amekaa usiku kucha pamoja Naye.

184 Yakobo angeweza kwenda kumlaki ndugu yake baada ya kukaa usiku kucha pamoja Naye. Hamkai muda mrefu vya kutosha, ndiyo shida, siku hizi. Mama zenu wazee na baba zenu wa kale huko Pentekoste waliomba mchana kutwa na usiku kucha, siku hizi, tunapiga magoti, "Mungu mbariki Mama na Baba, na dada na ndugu. Amina. Ninashikwa na usingizi sana sijui la kufanya. Sina budi kwenda nyumbani, niangalie kipindi kipya cha televisheni," mnaona, "kilichotokea. *Tunampenda Susie* kitachezwa baada ya kitambo kidogo," maskini kitu fulani cha ibilisi kilichopotoshwa, nafsi yako ikila kitu kama hicho, badala ya kuja kwenye mkutano wa maombi Jumatano usiku ama kitu kama hicho. Kisha umwite Mungu, akimwaga Roho Wake.

185 Anaweza kuangua nini? Kundi kubwa la madhehebu. Hivyo tu. Hiyo ndiyo aina ya mbegu iliyopandwa. "Vema, loo, mimi

ni mfuasi wa *hili*, nitaninii. . . " Loo naam. Afadhali niwe wa Mungu, hiyo ni kweli, naam, bwana, achana na mengine. Hiyo ni kweli.

186 Sasa, angalieni sasa, sasa, tunaona ya kwamba Yesu alishuhudia. Wakati Simoni, yeye alijua. . . a—akasema, "Ninajua yale baba yangu aliyoniambia, ya kwamba kutakuwako na machafuko mengi kote katika siku hiyo atakapokuja."

187 Ninaweza tu kumsikia maskini, mzee. . . Simoni akimwambia. . . baba ya—yake akimwambia mwanawe, kasema, "Mwanangu, angalia, nilitumaini kumwona Masihi, lakini nadhani ninazeeka sana sasa, sitamwona. Lakini sasa, sikiliza, ninataka ujue, sasa, kutakuwako na miigo mingi itakayoinuka, bali mtamjua huyo Masihi. Mnaona? Atakapokuja, Mwanangu, nimekufundisha jinsi ya kuvua samaki, nimekufundisha kuwa mwaminifu kwenye mizani yako huko chini, nimekufundisha kutimiza neno lako, hilo ndilo linalokufanya mtu mwadilifu, hilo ndilo linalokufanya mtu mwaminifu. Pia, Mwanangu, unaweza kuchukua mafundisho ya namna hiyo ukiwa mwaminifu, na kuamini neno la baba yako na uwe mwaminifu, kisha uwe mwaminifu na kuamini Neno la Mungu." Amina. "Mungu alisema Masihi huyu atakuwa ni Nabii, si mwanatheolojia, Nabii ambaye Bwana Mungu wako atamwinua."

188 Simoni alikuwa na jambo hili niani mwake. Siku moja wakati Andrea alipokuja kumwambia kuhusu, mbona, alikesha usiku kucha pamoja Naye, alishawishika. Naye Simoni anashuka kwenda kumwona Yule aliyekuwa akinena habari zake, siku hiyo ufukoni, wakati alipoketi kwenye kisiki hiki kidogo na kumsikiliza, lakini mara alipomtazama maskini Simoni, alisema, "Jina lako ni Simoni, nawe ni mwana wa Yona." Hiyo ilikuwa sawa. Hiyo ilikuwa sawa! Kwa nini? Alijua kulikuwa na ishara ya Kimaandiko, Huyo alikuwa ni Masihi.

189 Wakati Filipo alipoenda kumleta Nathanaeli, naye Nathanaeli akarudi, kasema, "Sasa, ngoja kidogo, huenda nimesikia habari zake, lakini nashangaa kama kweli ni kweli ama si kweli."

190 Akasema, "Ninii. . . ? Nisingejua, lakini ngoja mpaka utakapofika kule, utajionea. Simama na uangalie mkutano kwa muda kidogo uone kitakachotukia."

191 Hawa hapa Filipo na Andrea wakija pamoja, Yesu amesimama, akaangalia, akasema, "Tazama Mwisraeli kwelikweli, ambaye hamna hila ndani yake!"

Akasema, "Rabi," hilo lilimshusha papo hapo, mwajua, akasema, "Rabi, ulipataje kunijua?"

Akasema, "Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nilikuona." Ilikuwa ni kitu gani? Ishara ya Kimaandiko, Masihi. Hiyo ni kweli.

192 Yule mwanamke Msamaria, wakati alipokuwa kisimani, Yeye alisema, “Mwanamke, nipe maji ninywe.”

193 Akasema, “Si kawaida, tuna ubaguzi hapa, ninyi Wayahudi, na Wasamaria, hatuna uhusiano wowote. Nami ni mwanamke, Wewe ni Mwanamume, umekujaje kusema kitu kama hiki?”

Akasema, “Lakini kama ungalijua ni Nani unayesema naye, ungeniomba Mimi maji unywe.”

Akasema, “Mbona, tunajua, tunaabudu katika mlima huu, Ninyi husema huko Yerusalemu, Wewe ukiwa ni Myahudi,” na kadhalika, mazungumzo yakaendelea.

Yesu aliishika roho yake, akasema, “Nenda, kamwite mumeo, mje naye hapa.” Loo, jamani!

Akasema, “Sina yeyote.”

Akasema, “Umesema kweli.” Kasema, “Umekuwa na watano, na huyu wa sita uliye naye siye wako.” Kweli.

194 Alisema nini? Akasema, “Bwana, ngoja kidogo, kidogo tu, hapana shaka Wewe ni nabii, Hilo ni Neno la Bwana. Sasa, tunajua tunaishi katika siku ambapo tunamtarajia Masihi kuja, Naye atatuonyesha mambo kama haya.”

Yesu akasema, “Mimi Ndiye.”

195 Ndugu, kisima cha Yakobo hakikuwa na ladha tena, moja kwa moja akaingia mjini na kusema, “Njoni, mwone Mtu aliyeniambia yale ambayo nimefanya. Haimkini Huyo kuwa ndiye Masihi?” Ishara ya Kimaandiko ya kwamba Yeye alikuwa ni Masihi. Kweli kabisa. Naam, bwana. Naam.

196 Waliikataa. Watu walika-. . .Walimwitaje? Beelzebuli, mpiga ramli, ibilisi. Nini kilitukia? Waligaagaa katika damu yao wenyewe. Josephus anatwambia katika maandishi yake juu ya kuzingirwa kwa Yerusalemu na Tito, yule jemadari mkuu wa Kirumi, walipouzingira kule kwa miaka kadha, hata wakala magome ya mti, na kuwaua watoto wao kwa wao na kuwala. Ilikuwa ni kitu gani? Walikosa kuona ishara yao.

197 Yesu alisema nini? Alisema, “Enyi wanafiki, mmevaa mavazi haya yote ya kikuhani, na digrii za udaktari nyuma yenu, hawa akina ‘Papa John’ wote wakuu mno, na kadhalika, vyeo hivi vyote, na kadhalika, wanatembea barabarani na kutamani mahali pa juu, na mahali pazuri sana pa kwenda, wanakula nyumba za wajane, na kwa unafiki wa—wa—wanasali sala ndefu pamoja na. . .na kujifunza kuikariri,” Akasema, “mtapokea hukumu iliyo kuu zaidi.” Kasema, “Mnaweza kuangalia isha-. . . mnajua zaidi kuhusu—mnajua kuhusu sayansi kuliko mnavyojua Neno la Mungu.” Loo, ndugu, hilo—hilo liliwagonga.

198 Kasema, “Mnaangalia angani, na mnawasikiliza manabii wa hali ya hewa kuliko mnavyosikiliza Neno Langu. Mbona, mnasema kama anga imetanda na ni nyekundu, na kadhalika

namna hiyo, kwamba kesho kutakuwa na dhoruba, na kama jua linaangaza, kutakuwa na kianga." Akasema, "Mnaweza kuutambua uso wa mbingu, bali ishara za wakati hamwezi kuzitambua. Kama mngalinijua Mimi, mngaliijua siku Yangu." Hiyo hapo ishara, Masihi. Loo, jinsi, jinsi, jinsi walivyoshindwa vibaya! Jinsi ambavyo tungeweza kukaa hapa muda mrefu, lakini hatuwezi sasa, tunaninii, hatuna budi kuharakisha.

199 Sikilizeni, ndipo ikaja ahadi kupitia kwa Yesu, kile ambacho kingetukia kabla ya kuja Kwake. Sasa, hebu na tuchunguze hilo kwa dakika moja. Yapata dakika chache tu sasa, kidogo tu. Mmechoka? Kama mmechoka, mbona. . .Mnaona? Vema. Hebu na tuchunguze jambo hili kwa dakika chache. Sasa, sikilizeni kwa makini sana, tulieni. Sasa, tunaona ishara zote, tungeweza kukaa juu yake saa kadhaa, majuma, na miezi, pasipo kuliacha somo hilo moja, lakini hebu turudi moja kwa moja sasa, dakika chache tu, kisha turudi.

200 Sasa, Yesu aliulizwa, "Huo wakati utakuja lini ambapo halitasalia jiwe juu ya jingine? Na ni nini ishara ya kuja kwa mwisho wa ulimwengu? Utafika lini?"

201 Naye akaanza kuwaambia, "Injili hii itahubiriwa kwa kila taifa, ufalme, kwa ushuhuda Wangu." Mnajua nini? Sasa, Yeye kamwe hakusema. . .Yeye alisema, "Injili hii," sasa, Yeye hakusema, "Enendeni mkafundishe Neno," bali, "Mkaihubiri Injili," kuna tofauti nyingi, bila shaka. Injili ni nguvu na dhihirisho la Neno, mnaona, nguvu na madhihirisho ya Neno.

202 Mnakumbuka wakati yule Malaika aliposhuka mtoni, ambaye mna picha yake, na mnajua habari zake, wakati aliposema hapa kuhusu, katika mwaka wa 1933, nilipokuwa nikibatiza kundi langu la kwanza, kwamba Ujumbe ungeenea ulimwenguni? Na kila taifa, wana uamsho unaoendelea, wamekuwa nao kila mahali. Mnaona? Hakika. Kuwavuta Wateule watoke. Hiyo ni kweli. "Injili hii itahubiriwa."

203 Ndipo tunaona katika Ufunuo 3:1-3, kutakuwa na nyakati tatu za kanisa katika siku hizi za mwisho. Je, mlijua hilo? Hiyo ni kweli, tumekuwa nazo. Kumbukeni wanapopitia katika elementi hizo, kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu, Luther, Wesley, na Pentekoste, wale wajumbe watatu wa siku za mwisho, chunguzeni, kule kuja Kwake Mwenyewe katika nyakati za mwisho, tunaona jambo hili tena, ambapo tunaona kule kuja sasa kwa ninii Yake. . .mvua. . .Roho Mtakatifu akimwagwa katika siku za mwisho. Mnaamini amemwagwa? Juu ya nini? Mtu anapanda Mbegu apate kuzalisha Zao Lake la siku za mwisho. Mnajua Yoeli alisema, "Katika siku za mwisho. . . "

204 Sasa, angalieni, hili hapa jambo lingine ningetaka kulifikia, mnasema, "Ulianza tu na Wesley." Uliwahi kuwazia hilo? Nilipomaliza tu zile *Nyakati Saba za Kanisa*, hivi mliwahi kuona ni kwa nini alia-. . .Nilianza na Wesley? Kwa sababu

hapo ndipo lilipoanzia, la Wesley, baada ya yale matengenezo. Vipi kuhusu Mtakatifu Martin, na Mtakatifu Ireneo, na wale wote huko nyuma waliosimama wakipinga Kanisa Katoliki la Kirumi katika siku hizo, kudumu na Neno, walipoanza kwa mafundisho ya sharti? Ni kitu gani kilichoanzisha hilo? Ni kitu gani kilichowapata?

205 Hivi Yoeli hakuwaambia habari zake? "Yaliyosazwa na tunutu, yameliwa na madumadu; yaliyosazwa na madumadu, yu—yu—yule mwingine, yameliwa na nzige." Mnaona? Na mdudu yuyo huyo, kutoka tunutu, hata madumadu, hata nzige, na kadhalika, ni mdudu yule yule, ila tu katika hatua mbalimbali, na huo ni Ukatoliki. Ulifanya nini? Ukala Neno. Lakini Yeye alisema, "Nitarudisha, asema Bwana. Nitarudisha."

206 Inakuwaje? Likashuka moja kwa moja hata kwenye Kisiki. Hiyo ni kweli. Kanisa Katoliki la Kirumi lilikula kila kitu ambacho Biblia inafundisha. Kweli. Walijitengenezea mafundisho yao ya sharti ya Kirumi kutokana nayo, hata ushirika wao, roho wao mtakatifu wa uongo, ubatizo wa uongo, ubatizo wa uongo wa maji, kila kitu kingine. Kamwe, kamwe, kamwe hutakuwa sawa mpaka utakaporudi kwenye Uzima, unaotoka kwenye Kisiki, na Hilo ni Neno la Mungu. Watu wapate kuwa huru, liliwafunga katika madhehebu na kuwachoma moto, na kuwaua, na kuwalisha simba, kila kitu kama hawakujiunga nalo. Hiyo ni kweli kabisa.

207 Lakini Yeye alisema hicho Kisiki kitakua tena, kitachipuka. Kitu cha kwanza kutokea kilikuwa nini? Kilikuwa ni mti. Ni kitu gani kinachofuata? Majani. Ni kitu gani kinachofuata? Maua. Ni kitu gani kinachofuata? Tunda. Luther, Wesley, majani; Pentekoste, maua. Sasa, tunaelekea moja kwa moja kwenye tunda. Kanisa linafifia. Amina.

208 "Nitarejesha," asema Bwana. "Nitafanya nini? Nitalirudisha kwenye hali yake ya asili. Nitalirudisha kwenye Fundisho lake la asili. Nitamrudisha kwenye Neno la asili. Nitavunja kila dhehebu vipande-vipande. Nitalirudisha kwenye Neno Langu." Namna gani? Labda afadhali ninyamaze. Naam, nisimame, Jamani. "Nitalirudisha."

209 Dhehebu la kwanza lilikuwa ni lipi? Ulizia. Kanisa Katoliki. Kweli kabisa, uko sahihi kabisa. Vema, linaitwa katika Biblia, katika Ufunuo 17, kahaba. Hiyo ni. . .Mwanamke wa namna hiyo, loo, ni nini? Ni mwanamke asiye mwaminifu kwa mumewe. Mnaona? Hilo ni kanisa ambalo si aminifu kwa Neno. Naye alikuwa mama wa makahaba. Kahaba ni nini? Kitu kile kile. Tutafikia jambo hilo, sawa tu, yapata tu dakika mbili zaidi, tatu. Mnaona? Vema.

210 Haya basi, yeye ni mama wa makahaba, kitu kile kile alichokuwa, likiunda madhehebu, likiondoa Fundisho la Biblia, likijifundisha lenyewe, likifundisha Mafundisho yaliyo amri za

Mungu, na kuzitangua amri za Mungu kwa mapokeo yao. Yesu alikabiliwa na jambo lile lile. Chungu hakiwezi kusema birika ni nyeusi. Hiyo ni kweli. Zote zinafanana. Naam, bwana.

211 Unapoondoka kwenye Neno hilo, umemwacha Mungu, umeziacha kanuni, umemwacha Roho Mtakatifu, umeondokea kila kitu. Ibilisi atakupa kitu cha uongo, bali kamwe hatakishuhudia. Mpaka iwe ni kweli, rudini moja kwa moja kwa Masihi yuyo huyo, Huyo ni Roho wa Mungu, "Mimi ni Mzabibu, ninyi ni matawi." Uhai ule ule ulio ndani ya mzabibu uko kwenye tawi, nalo tawi huzaa tunda la mzabibu, Yohana Mtakatifu 15.

212 Vema. Walifanya nini? Sasa, hao wote, mwajua, Yesu alisema katika siku za mwisho Yeye angefunga, kwanza Yeye angeyafunga nini yote? Magugu. Hiyo ni kweli? Jamani, hakika wanayafunga sasa, Baraza la Makanisa Ulimwenguni lina kila mmoja wao, Wapentekoste na wote. Yote yamefungwa pamoja yapate kuteketezwa, hiyo ni kweli kabisa. Um-hum. Kuwatenganisha na Ngano, Mungu asifiwe kwa ajili ya jambo hilo. Hiyo ni kweli, kuwatenganisha wote, wasioamini. Usitembee katika njia yao, usiende kwa masomo yao, njoo kwa Neno. Kweli. Usifadhaishwe na ishara za Mungu, ishara za kweli za Mbinguni. Hizo ni, si ishara za. . . Ishara za Mbinguni, si ishara za kanisa, ishara za Mbinguni, ishara zilizotumwa na Mungu, usifadhaishwe nazo, dumu nazo. Unaona? Vema.

213 Baraza la Makanisa likiungana pamoja, wanafanya nini? Wanatimiza Ufunuo 13, "Nao wakafanya sanamu ya mnyama." Sanamu ni nini? Tunajua i—ile sanamu ni nani, yule joka aliyesimama mbele ya yule mwanamke apate kumla yule Mtoto, Mtoto mwanamume aliyekusudiwa kuutawala ulimwengu kwa fimbo ya chuma, Kristo. Naye akanyakuliwa hata Mbinguni, akaketi kwenye Kiti cha Enzi cha Mungu. Lile joka lililosimama mbele ya huyo mwanamke, huyo ni mnyama yule yule hapo mwanzo, Rumi. Yeye hufanya nini? Anawaweka watu pamoja. Nao wakafanya sanamu.

214 Papa John anayataka makanisa yote yakusanyike pamoja kupiga vita ukomunisti. Naye Mungu, mtu yeyote anayejua Biblia anajua ya kwamba Mungu aliunda ukomunisti autumie kumwua, kumchoma moto, kumchukia huyo kahaba, na kumteketeza, watoto wake katika kitanda cha moto, hakika, kabisa. Anautumia kama tu alivyomtumia Mfalme Nebkadreza.

215 Nayo makanisa ya—ya Kiprotestanti yataungana pamoja na kufanya baraza la makanisa, nao Wapentekoste moja kwa moja pamoja nao. Kwa nini? Hawalijui Neno. Hiyo ni kweli kabisa, Neno linaahidi hilo.

216 Mungu, mtume mtu akakilipue kitu hiki, akawaonye watu. Tuko moja kwa moja katika saa hiyo, papa hapa sasa, hiyo hapo siku, tunaangalia hapa, tunaona ishara, jamani, ziko kila mahali

juu yetu, kila mahali. Unashangaa kuna nini, kwa nini kanisa halijaingia kwenye Unyakuo? Vema, kamwe halitaingia namna hiyo, halitaingia. Hiyo ni kweli. Hilo silo Lile alilokuwa akinena habari zake.

217 Kumbukeni, bibi-arusi wa Adamu alikutwa na uzao wa uongo. Hiyo ni kweli kabisa. Bibi-arusi wa Yehova alipatikana vivyo hivyo, kweli, Yeye alimtaliki na kumwacha. Hiyo ni kweli? Huyo alikuwa ni Mungu.

218 Bibi-arusi wa Kristo ni kitu kile kile, anapatikana akiwa na mbegu ya kimadhehebu ya kilimwengu ndani yake wala si Injili, akiwa na mfano wa utauwa lakini akikana nguvu zake zitokazo kwa Roho Mtakatifu na Neno. Hiyo hapo ishara ya siku ya mwisho. Mungu atampa talaka na kumchukua Bibi-arusi Wake, hakika kabisa kama chochote humu ndani. “Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu,” Yeye alisema, “ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.”

219 Angalieni, wakifanya sanamu ya mnyama, tunaona haya yote. Rais mwenyewe Mkatoliki, si Kennedy, kadiri nijuavyo yeye ni mtu kama nilivyo mimi au mtu mwingine yeyote, si huyo. Haikuwa Ahabu, Ahabu alikuwa ni jamaa mzuri sana, ilikuwa ni huyo Yezebeli nyuma yake, huyo ndiye aliyekuwa nyuma yake, hicho ndicho kitu kilichosababisha shida. Wala si Kennedy, ni lile kanisa la Yezebeli lililo nyuma yake, hilo ndilo linalofanya hivyo. Hakika, hivyo ndivyo hasa.

220 Ni, mbona, jambo hilo liko moja kwa moja mbele zenu. Hivi hamwezi kuona ninii—hivi hamwezi kuona ninii, kila kitu...? Kuona mtini ukichipuza matawi yake? Yesu alisema, “Mtakapo-...Jifunzeni mfano: Mtakapouona mtini, na miti mingine yote...” Sasa, angalieni, Wayahudi wameanzisha uamsho, tayari wanakuwa taifa. Hiyo ni kweli? Pesa zao wenyewe, bendera yao, kila kitu, mara ya kwanza kwa muda wa miaka elfu mbili mia nane. Mnaona? Wao ni taifa. Mtini, unachipusha majani yake.

221 Na mti huo mwingine, Wabaptisti, “Milioni moja zaidi katika mwaka wa ’44,” Billy Graham akilichinja kutoka upande mmoja hadi mwingine, “Ninyi nyote njoni mkajiunge, njoni mkajiunge, njoni mkajiunge.” Wapentekoste, jambo lingine. Umoja, Uwili, Utatu, Assemblies, kila kitu kingine, “Njoni mkajiunge, njoni mkajiunge, njoni mkajiunge.”

222 Ee Mungu! Yako wapi mambo ambayo Mungu aliahidi? Yako wapi? Yako wapi yale mambo ya Kimaandiko ambayo Mungu alisema yangetukia katika siku za mwisho? Yako wapi? Hatuna kitu ila kundi kubwa la madhehebu baridi, ya kawaida. Uamsho umewaingiza kwa maelfu katika kila moja la hayo, lakini yuko wapi Bibi-arusi yule wa Kristo anayesimama katika usafi? Wanawake wetu wote wakikata nywele zao, na kuvaa nguo za kila namna, na wahubiri na kadhalika hawasemi neno

juu yake, huku—huku wakitoka nje na kuwa wa kawaida na wasiojali, nayo Injili imekuwa ni njia ya riziki, kama ilivyo kwa hawa wahubiri wengine wa Injili ya kijamii.

223 Tunachohitaji ni mtu wa Mungu atakayelitetea Neno la Mungu, na kulihubiri bila kujali, na kusimama hapo na ishara pamoja na maajabu ya Biblia ya Mungu. Hiyo ni kweli kabisa. Amina. Kweli kabisa. Wanaogopa kuita cheusi, "cheusi," na cheupe, "cheupe," mfupa wa shingo ya kuku badala ya uti wa mgongo. Ni—ni aibu. Wa kisasa, huru, na, loo, jamani, halafu basi. . . Jamani, afadhali ninyamaze.

224 Sikiliza, hebu nikwambie, ndugu, ishara zimekuzunguka kote. Usihofu, ewe Bibi-arusi mdogo, Mungu yuaja, usihofu, kila kitu kiko katika wakati ufaao. Hili halina budi kutukia namna hii, Neno linasema hivyo.

225 Sikilizeni, angalieni, sasa, Yesu aliahidi ya kwamba kizazi hiki kiovu na cha zinaa, Mathayo 12:24, Yesu aliahidi ya kwamba kizazi hiki kiovu na cha zinaa kingepata ishara. Walimjia, wakasema, "Bwana, sisi tunataka kuona ishara kwako," mara baada ya kuwa akiwaponya wagonjwa, na kufanya mambo yale aliyokuwa amefanya. Kasema, "Tunatafuta ishara kutoka kwako." Yeye alisema, "Kizazi kiovu na cha zinaa chatafuta ishara, wala hakuna ishara itakayopewa kizazi hicho kiovu na cha zinaa. . . "

226 Ni wangapi wanaojua ya kwamba utovu wa uadilifu umeenea sana kuliko ulivyowahi kuwa? Ni wangapi wanaojua ya kwamba uovu ni kutokuamini? Kutokuamini kwingi na uzinzi mwingi zaidi kuliko tulivyowahi kuwa nao, walawiti, kila kitu kingine. Hiyo ni kweli? Upotovu.

227 Si—si—sina budi, si—sina budi kulisema, wanawake wetu wa Kipentekoste, wakijichuna ngozi kwa maskini nguo chafu kama mnyama aliyechunwa ngozi, wakitembea hapa nje mtaani kwa utovu wa uadilifu. Je, mlijua mtajibu kwa kufanya uzinzi? Hao wanaume wakiwaangalia, nanyi mkiwaweka watoto wenu nje namna hiyo. Kuna nini?

228 Mbona, vema mtu fulani alisema si muda mrefu uliopita, kasema, "Ndugu Branham, watu wanakuita nabii."

Nikasema, "Mimi si nabii."

229 Kasema, "Vema, watu wanakuita hivyo. Kwa nini usiwafundishe mambo makuu, jinsi ya kupokea karama za Mungu, badala ya kuzungumza na wanawake kuhusu kukata nywele, na—na kuvaa vitu jinsi wanavyofanya, na kujipodoa na vitu wanavyofanya, na mambo kama hayo?"

230 Nikasema, "Nitawafundishaje aljebra kama hawatajifunza ABC zao?" Naam. Hawatatoka kwenye shule ya chekechea, ile adabu ya kawaida kujilainisha na Neno la Mungu, kweli kabisa. Utafanyaje jambo hilo? Huwezi kufanya hivyo.

231 Kwa nini? Wale tu Mungu aliowaita ndio watakaoisikia, "Kondoo Wangu huisikia Sauti Yangu." Hiyo ni kweli. Wanaijua Sauti ya Mungu, inanena kutoka kwenye Neno. Neno ndilo linalofanya jambo hilo.

232 Sasa, Yeye alisema kizazi hicho, ndicho *hiki*, kingepokea ishara. Ishara ya namna gani? "Kama vile Yona alivyokuwa katika tumbo la nyangumi siku tatu, Mwana wa Adamu atakuwa katika moyo wa nchi."

233 Hiyo ni kweli? Wangepokea ishara ya namna gani? Ishara ya ufufuo. Yesu hajafa, Yeye yu hai. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Hiyo ni kweli? Kizazi kiovu na cha zinaa kingepokea ishara ya ufufuo. Amina. Wangejaribu kuipinga. Walifanya hivyo, walimfanyia Yeye. Mathayo, ukitaka kuandika hilo, Mathayo 13:24, walifadhaishwa sana nayo.

234 Wakasema, "Jamaa huyu, inatubidi kuyajibu madhehebu yetu, sisi Mafarisayo hatuna budi kuwajibu, Masadukayo, na Maherodia, watoza ushuru, na kadhalika, sote hatuna budi kulijibu hili. Ni kitu gani? Mbona, yeye ni mpiga ramli, hiyo ndiyo sababu anajua kilicho mioyoni mwao, alitambua mawazo yao, yeye ni mpiga ramli."

235 Alisema kamwe hakuna msamaha kwa hilo wakati jambo hilo litakapotukia katika siku za mwisho. Hiyo ni kweli. Wakamwita Beelzebuli, mkuu wa pepo. Hiyo ni kweli. Hawakupendezwa Naye. Hiyo ni kweli? Lakini Yeye aliliambia Kanisa, hili Kanisa halisi hapa, "Msife moyo kwa ishara hizo za Mbinguni, kwa kuwa waovu, makafiri, wasioamini wanavunjwa moyo nazo," Mnaona? Nasi tuko katika siku za mwisho.

236 Hebu tufunge kwa kusema jambo hili, kwa muda kidogo tu: Nao wanasema sivyo ilivyo, wanasema tu ya kwamba hivyo sivyo Mungu alivyolifanya, "Mungu anataka *hili* kubwa mno, na *lile* kubwa mno, nasi tutajenga, dola milioni sita, na tutaweka *hili* katika *hili*, na *hili* katika *lile*," huku wakihubiri Mwana wa Mungu yuaja mara moja.

237 Ni kitu gani? Yote yamegeuzwa kuwa chakula cha kimadhehebu, yamefungwa katika kundi kubwa la muungano wa makanisa, yapate kuchomwa moto wakati wa mwisho, kasema, yale Yesu aliyosema. Aliona michongoma na vitu vya kila namna vimefunganishwa nayo, hiyo ni kweli, kuzozana, kupiga makelele, kuzuia uamsho usiingie nchini.

238 Ninampa changamoto mtu huyo aliyenipa changamoto kwa Neno hilo, mtu mwingine yeyote. Bishana Nalo uone kitakachotukia, um-hum, uone kitakachotukia. Kama huwezi kulivumilia, basi nyamaza, hiyo ni kweli. Ama njoo ujirekebishe, au tuseme, ufanye jambo fulani. Naam, bwana.

239 Nuhu, Mathayo 24, tunaona hizo siku zikitimia. Pia kumbukeni, Yesu alisema, pia, katika Luka Mtakatifu 17:28 hadi 30, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo

itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu." Hiyo ni kweli? Sasa, kumbukeni, Sodoma ilikuwa . . . kabla tu ya Sodoma kuteketezwa, nao walipokea nini? Wanapata ishara? Hakika.

240 Sasa, kuna matabaka matatu ya watu daima, sasa, kumbukeni, hao ni wasioamini, wanaojifanya waaminio, na waaminio. Kuna ishara tatu, matabaka matatu, daima yamekuwako, yalikuweko papo hapo. Sasa, angalieni, Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma . . ." Namna ile ile, jambo lile lile. Mnaona? Aliendelea, akawaambia waliyokuwa wakifanya katika siku za Nuhu, wakila, wakinywa, wakioa, wakiolewa.

241 Kasema kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma kabla ya kule kuteketezwa. Sasa, angalieni yaliyotukia kabla ya hukumu. Sasa, Yeye atatuma ishara kwa kizazi hiki kabla tu ya wakati wa kuteketezwa, hakuna maji tena, ila nini, wakati huu? Moto. Hukumu za Mungu, zitakuwa ni Moto. Nayo Sodoma ilipokea nini?

242 Sasa, kabla tu ya kule kuteketezwa, Ibrahimu aliwakilisha Kanisa teule, kwa sababu aliteuliwa, Ibrahimu aliteuliwa. Nao Uzao wa Ibrahimu umeteuliwa pamoja naye. Ahadi ilifanywa kwa Ibrahimu *na* Uzao wake, Uzao wake wa kiroho, Uzao uliokuwa ndani yake uliolipokea Neno la Mungu. Haidhuru ni kitu gani kingine kilichoenda kinyume Nalo, bado ni Neno la Mungu, Yeye alidumu moja kwa moja Nalo, huo ni Uzao wa Ibrahimu, Ule unaodumu na Neno, si hao wanaokimbia kama Lutu. Unaona?

243 Kulikuwako na Wasodoma, wasioamini; kulikuwako—kulikuwako na Walutu, walikuwa ni waaminio wa kujifanya; na huyo hapo Ibrahimu, ile ahadi, mteule, mwaminio.

244 Malaika watatu walikuja katika hema la Ibrahimu siku moja. Wawili wa Hao walishuka na kuhubiri ujumbe mzuri kwa Wasodoma, nao wakaita kundi fulani litoke. Lakini haikuwabidi kumwita Ibrahimu atoke, kwa sababu tayari alikuwa ametoka, hakuingia mle, kwanza kabisa. Alikuwa ameondoka miaka ishirini na mitano kabla ya hapo. Naam, bwana. Aliitwa atoke, mteule, aliyeitwa atoke, ameketi huko nje jangwani. Ndipo basi hao wengine wakashuka, wakahubiri Injili kule chini, na hatimaye wakatoka kwa shida wawili au watatu.

245 Ujumbe umeenda Sodoma, kumekuwa na baadhi ya makanisa katika madhehebu hayo, wengi wao wameokolewa. Vema, kumekuwa na Ujumbe waliopewa Wateule pia, Neno, ile ishara. Mnaona?

246 Huyu alisema, yule Msemaji aliyenena na Ibrahimu alisema . . . Sasa, kumbukeni, yeye alikuwa Abramu siku nne ama tano kabla ya hapo, naye Sara alikuwa S-a-r-r-a, sio S-a-r-a-h. Alikuwa A-b-r-a-m, sio A-b-e-r-h-a-m, mnaona, siku nne au tano tu kabla ya hapo, mnakumbuka. Ndipo Mtu

huyu akaja na kusema, “Ibrahimu, yu wapi Sara, mkeo?” S-a-r-r-a, S-a-r-a, hasa. “Yu wapi Sara, mkeo?”

Mbona, Ibrahimu akasema, “Yuko—yuko hemani, Bwana, nyuma Yako.” Sasa, Biblia ilisema nyuma Yake.

247 Akasema, “Ibrahimu, sitakuficha jambo hili tena. Nilikupa ahadi.” Mnaona Yeye alikuwa ni Nani? Yule aliyekuwa akizungumza naye wakati wote, mnaona, Yule aliyekuwa pamoja naye. Mnaona? “Nilikupa ahadi, nitaitimiza. Kwa muhula wake nitakurudia, Sara atarudi kuwa kama msichana, na kadhalika, nawe utamzaa huyu mwana.” Mnaona?

248 Sasa, hiyo ilikuwa ni ishara ya kwamba mwana aliyeahidiwa tu alikuwa yuaja. Mnaona? Ibrahimu alikuwa akimtazamia mwana aliyeahidiwa. Hiyo ni kweli? Je, Kanisa linamtazamia Mwana aliyeahidiwa? Kweli? Ishara ya mwisho aliyopata Ibrahimu ilikuwa ni nini? Alisema, “Nitakuzuru kuli-. . . ”

249 Naye Sara, akiwa hemani, akacheka kifichifichi, akasema, “Mimi, mwanamke mkongwe, nipate raha na bwana wangu, Ibrahimu, yeye akiwa mzee pia?” Sasa, wote wawili walikuwa na umri mkubwa, sasa, mke alikuwa na tisini, naye mume alikuwa na mia moja, hawakuwa mume na mke kwa miaka mingi. Mnaona? Kasema, “Nipate raha na bwana wangu, naye ni mzee pia, namna hiyo, nami ni mzee?”

250 Biblia ilisema ya kwamba mwili wa Ibrahimu ulikuwa kama uliokufa, hiyo ni kweli, nalo tumbo la uzazi la Sara lilikuwa limekufa, “Lakini hakusita katika ahadi ya Mungu kwa kutokuamini, bali alitiwa nguvu, akimtukuza Mungu, alijua ya kwamba yale aliyoahidi atayafanya.” Hivyo ndivyo itupasavyo. . . Uzao wake unafanya jambo lile lile, Uzao wake ulioahidiwa, Uzao wa Kifalme, unaamini jambo lile lile.

251 Sasa, angalieni, papo hapo Yeye akasema. . . naye akacheka, Yeye akasema, “Kwa nini Sara akacheka?” Hiyo hapo ishara Yake, hiyo hapo ishara kwa Kanisa, Kanisa lililoitwa litoke: Mwanadamu, Mwanadamu, mwili wa mwanadamu, akila vipande vya nyama ya ndama, ugali wa mahindi, na kunywa maziwa. Je, alifanya hivyo? Ilikuwa ni Mungu? Angalieni kama sivyo. Angalia katika Biblia yako uone kama haionyeshi, “Elohimu.” Elohimu, yule Aishiye Peke Yake, Elohimu, katika mwili wa kibinadamu. Ni ishara ya nini? Elohimu, amerudi katika Bibi-arusi, mwili wa kibinadamu tena, katika siku za mwisho akifanya jambo lile lile. Iko wapi? Hiyo hapo ishara yako kwa ajili ya siku za mwisho.

252 Katika Zekaria 14:7, ilisema, “Kutakuwa na siku isiyoweza kuitwa mchana, wala usiku,” ni siku yenye utusitusi, yenye mvua kama vile tumekuwa nayo leo, yenye utusitusi, yenye mvua, “lakini wakati wa jioni itakuwa Nuru.” Sasa, kama nilivyosema mara nyingi, ustaarabu unatoka mashariki ukienda magharibi, jua lile lile linalochomoza mashariki hutua magharibi. Imekuwa

ni siku ya madhehebu, tumekuwa na Nuru ya kutosha kujenga makanisa, na shule, na hospitali, na seminari, na kadhalika, tulikuwa na Nuru kidogo, tukamkubali Kristo na kuandika jina letu kwenye vitabu, na kadhalika namna hiyo.

253 Lakini Yeye alisema, "Wakati wa jioni itakuwa Nuru." Ni kitu gani hicho? Nuru ya Injili. Hiyo inafanya nini? Roho Mtakatifu. Inafanya nini? Inayaivisha Mazao. Katika siku za mwisho Roho Mtakatifu atamwagwa katika wakati ufaao, katika siku za mwisho, kuleta mvua ya vuli, mvua halisi. Lakini kwanza, utapataje mvua wakati tungali tunapanda mbegu za kimadhehebu, tukiingiza kutokuamini zaidi wakati wote? Mbona usipande Mbegu ya Injili, ulete nguvu za Mungu katika ufufuo. Hizo hapo ishara za siku za mwisho. Hii ndiyo ahadi Yake, marafiki.

254 Angalieni hapa, hebu tuchukue tu ishara tatu, sasa hivi, pamoja, tufanye tatu katika thibitisho, ninaweza kuwapa dazani moja ya hizo. Siamini ya kwamba kuna kitu kama vitu hivi mnavyosema, vema, kama zodiaka, na kama mafundisho ya piramidi, vitu. Sitazungumzia hilo kwa sababu kuna kitu fulani mle ndani ambacho, muda si muda mwajua, unajifunga katika Waingereza Waisraeli, na upuuzi huo wote, ambao hauna chochote.

255 Lakini hebu niwaambie, kulikuwako, Biblia ya kwanza iliyowahi kuandikwa ilikuwa angani. Angalia zodiaka. Inaanza na nini? Bikira, Kuja mara ya kwanza kwa Kristo, inashuka kupitia kwa samaki waliokingamana. Ni kitu gani hicho? Wakati wa Kaa. Ndio kwanza tuupitie. Na ni kitu gani kinachofuata? Leo, yule simba, kule Kuja mara ya pili, kama Simba wa kabila la Yuda.

256 Angalieni zile piramidi, jinsi zilivyoanza, sehemu kubwa ya chini hapa, huo ulikuwa ndio mwanzo wa Kanisa. Ilikuwa ni kitu gani? Ya kwanza ilikuwa ni ya Kilutheri, katika yale matengenezo ya kulijenga Kanisa. Mstari wa pili ikawa zaidi katika uchache, Wesley akaja akihubiri utakaso. Ndipo baada ya huo kuendelea, likapiga hatua zake, kama ule mti, kwanza ilikuwa ni punje ya mahindi, ikaingia ardhini, iliyofuata ilikuwa ni majani, hiyo nyingine iliyojitokeza ilikuwa ni nini? Kishada. Ndipo ni kitu gani kilichofuata? Mahindi yale yale, Uhai ule ule, "Nitarudisha, asema Bwana." Iliyofuata ilikuwa ni suke la mahindi, kitu kile kile kwenye mti. Hicho ndicho Mungu amekuwa akikuza. Yeye . . .

257 Baadhi ya Wapentekoste siku hizi hata hawamhesabu Martin Luther na hao wengine, kwa sababu wanasema hakuwa na Roho Mtakatifu; alikuwa Naye. Huenda hakuwa Naye katika kilindi tunachompata sasa, lakini hakuwa kwa ajili ya wakati huo. Msipige makelele, huenda tukafikia kitu fulani kinachonata

katika dakika chache. Mnaona? Kwa hiyo mnaona, na Wesley, na hao ndugu, hakika walikuwa.

258 Lakini ilikuwa ni kitu gani? Ilikuwa ni—ilikuwa ni Mwili, ukikua kutoka miguuni, ukipanda juu, sehemu muhimu zaidi za Mwili zinatokea kutoka miguuni, hadi kwenye mapafu, na moyo, na kuingia Kichwani. Kichwa ni nani? Kichwa ni nani? Kristo. Hiyo ndiyo Akili. Jinsi, Mwili husonga namna gani? Kwa Kichwa. Amina. Na serikali itakuwa juu ya nini? Nini Yake. . . [Kusanyiko linasema, "Mabega."—Mh.] Mabega Yake ni nini? Mwili Wake. Amina.

259 Hapo ndipo Kanisa halisi la kweli linaponena katika nguvu Zake. Hapo ndipo nguvu za kimitume zinaporudi Kanisani, wakati serikali itakapokuwa mabegani Mwake, hukumu. Kanisa halisi linakuja, ninaamini, nikijaribu kufanya sehemu yangu kuliwasilisha, kuliweka tayari vizuri nijuavyo, kuwasilisha sehemu yangu, katika wakati wangu, kwa Kristo atakapokuja.

260 Angalieni, na nini. . .? Je,. . .? Kama una noti ya dola moja mfukoni mwako, itoe. Upande mmoja, upande wa kulia, ina muhuri wa Marekani, tai mwenye mishale kwenye makucha yake, huo ndio muhuri wa Marekani. Halafu upande huo mwingine una piramidi, wala kifuniko kamwe hakikuwekwa kwenye piramidi, ina kitu kama jicho kubwa linaloangaza pale kama kifuniko, nayo inasema "Ule Muhuri Mkuu."

261 Kwa nini huo uwe ndio Muhuri Mkuu Marekani badala ya muhuri wetu wenyewe? Umewahi kuliwazia? Iangalie, uone kama haisemi, "Ule Muhuri Mkuu." Kwa nini piramidi haikuwahi kuwa na kifuniko juu yake? Jambo lile lile liko katika hekalu la Sulemani, lile jiwe la kichwani lilikataliwa. Bila shaka. Lakini linashuka.

262 Nami nimekuwa kwenye piramidi huko Misri, nayo mawe yamelazwa mle ndani kikamilifu sana hata huwezi kuchukua wembe, ni vigumu, na kuuingiza kati yake. Sasa, yanaumana kikamilifu, jinsi walivyoijenga, hawajui, na sfiniksi na kadhalika, hawawezi kujua. Lakini angalieni, papo hapo ambapo jiwe hilo la kichwani linapopaswa kutoshea, pamechongoka. Kama kamwe wangeweza kupata lile jiwe la kichwani, lingeenea kikamilifu sana na vizuri, lingekifunga kitu hicho chote pamoja. Huyo ni Bibi-arusi wa Yesu Kristo. Wakati lile Jiwe la Kichwani litakapokuja, kutakuwako na Kanisa hapa duniani litakalolipokea, Ambalo litakuwa na huduma kama Yake kabisa, Litaingia tu moja kwa moja mle ndani, likiileta miguu, Luther, hao wengine wote, kwa ajili ya ufufuo.

263 Wengine walilala mauti katika zamu moja, wengine katika zamu iliyofuata, na wengine katika. . .kushuka hata zamu ya saba, hizo ni zile nyakati saba za kanisa, lakini Bwana-arusi alipokuja waliamka, amina, akaja kutoka chini. . .kutoka

miongoni mwa wafu, akafufuka katika ufufuo. Tunaishi katika siku za mwisho.

264 Unasema, "Ati ulisema nini? Luther, Wesley, kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu?" Naam. Halafu lile Jiwe la Kichwani. Hiyo ni kweli? Jiwe la kichwa lilikuwa katika ile piramidi.

265 Hebu tuchukue safina. Hebu tuichukue, hii hapa moja. Hebu tuondoke kwenye sehemu hiyo, turudi hapa. Hebu tuchukue safina, ghorofa moja, ghorofa mbili, ghorofa tatu. Hiyo ni kweli? Nuru ilitokea wapi? Dirisha lilikuwa wapi? Ghorofani, kwenye ghorofa ya tatu. Hapo ndipo nguvu za Mungu zitakapokuja kwa Kanisa. Jua, j-u-a, liliangazia pale, lakini M-w-a-n-a ataingilia *hapa* kwenye Kanisa ambalo Mungu analichonga na kuliweka tayari, akileta huduma Kanisani, kama tu vile tunutu alivyofanya, na—na nzige, na madumadu wakala huko nyuma.

266 Kisiki hiki kimekua kutoka Wesley hadi . . . kutoka Luther, hadi Wesley, hadi Pentekoste, na sasa kuwachonga hao Wapentekoste, na wale walio na ubatizo wa Roho Mtakatifu, naye atakuja, siku moja, lile Jiwe la Kichwani, Kristo Yesu, katika siku hizi za mwisho. Nasi itatubidi kuwa na huduma inayofanana kabisa na Yake, Roho Yake yote inapozidi kukaribia zaidi, zaidi, zaidi. Negativu inakuwa halisi sana hata baada ya kitambo kidogo Negativu na Halisi zinachanganyikana, Kanisa na Kristo kufanyika Mmoja, kwa kuwa sisi ni nyama ya nyama Yake na mfupa wa mfupa Wake. Amina. Mnaamini hilo?

267 "Itakuwa Nuru wakati wa jioni." Amina. Tupo hapa leo. Mnaamini hilo? Samahani kwa kuwaweka muda mrefu hivi. Na tuombe.

268 Baba yetu wa Mbinguni, sasa tuko mwishoni mwa mahubiri, mwishoni mwa muhtasari huu, mwishoni mwa huu ujumbe wa usiku. Nami nilijaribu kusema, kwa njia yangu iliyovunjika-vunjika, Bwana . . . Na yale nisiyoweza kusema katika Neno, Wewe—Wewe yafanye halisi kwao. Huenda nikasema yale uliyosema hapa katika Neno, bali kamwe siwezi kulifanya liishi, itahitaji Wewe kulifanya liishi, Bwana. Hiyo ni ile Mbegu, sasa itie maji, Bwana, ninaiwasilisha Kwako, katika Jina la Yesu Kristo.

269 Tujalie, Baba, kwamba tutaona Neno likithibitishwa kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, kama ilivyokuwa kwa Bwana wetu. Kama ni Masihi ajaye, nasi ni Masihi wadogo waliozaliwa mara ya pili, kama wana wa Mungu, tuliofanywa wana wenye mamlaka, itambidi kuingia Kanisani Mwake apate kuwa nyama ya nyama Yake, na mfupa wa ninii Wake . . . wa mfupa Wake.

270 Ninaomba, Mungu, ya kwamba utajidhihirisha Mwenyewe, usiku wa leo, na kuonyesha mambo haya kuwa ni kweli, kwamba mchungaji huyu mpendwa, kanisa hili la kupendeza, watu hawa wapendwa, wote wapate kubarikiwa na kujua ya

kwamba ishara za wakati wa mwisho ziko hapa. Jambo lile lile ambalo. . .Mbona, haikuchukua muda mrefu hata yule mwana aliyeahidiwa akatolewa, mara maskini Isaka akajitokeza jukwaani baada ya ishara hiyo kufanywa kwa lile Kanisa lililoitwa litoke, yule Uzao wa Kifalme, yule Uzao mwenye ahadi. Ila, Lutu alikuwa tu wa jamaa ya huo Uzao.

271 Bwana, tunaona makanisa ya kawaida, yasiyojali, siku hizi, yakijiundia madhehebu, Presbiteri, Methodisti, Baptisti, yote pamoja, wengi mle ndani ni wanawali, na wengi wao wanajaribu kutoka sasa, Waepiskopolia, na kadhalika, wakijaribu kutafuta, na ndugu zetu wa thamani, wengi wa ndugu zetu Wapentekoste, wakiwaendea na kulifurahia, bila shaka tutafanya hivyo, Bwana, lakini je, hao watu kweli wanaelewa ya kwamba wakati ule ule ambapo mwa—mwanamwali aliyelala alikuja kununua Mafuta, hapo ndipo Bwana-arusi alipokuja?

272 Loo, Bwana, liamshe Kanisa upesi sana, Bwana, nami nina hakika utafanya hivyo, lakini Wewe ulisema wakati mmoja, ulipoyaangalia mavuno, na kusema, "Watenda kazi ni wachache. Mwombeni Bwana wa mavuno, kwamba apeleke watenda kazi katika mavuno Yake." Sasa, Baba, tunajua ya kwamba Wewe unataka tuombe. Sisi ni wenzako, inabidi iwe ni sisi pamoja, tunatambua ya kwamba hata Malaika hawezi kufanya hivyo, inahitaji watu.

273 Filipo alitumwa kwa yule towashi, bila shaka, Bwana, yeye alitumwa kule na Malaika, lakini ilihitajika mikono ya Filipo. Hakika, tunatambua ono lilimjia Paulo akienda zake Dameski, bali ilihitaji mikono ya Anania, Kanisa, aliyeitwa atoke, mteule. Petro alitumwa kwa ono hadi kwa Kornelio, lakini ilihitaji mtume, si ono, si Malaika.

274 Mungu, ninaomba, usiku wa leo, ya kwamba Wewe utawaamsha watu, na uwajalie waone ya kwamba ahadi iko hapa, nayo ilitolewa kwa Kanisa hilo, "Wowote mtakaowaondolea dhambi, wameondolewa." Bwana, tunajua kuna wengi wao wanaoidai, bali wao ni mitume wasioidhinishwa kwa sababu wao si wa kimaandiko.

275 Tunaomba, Mungu, ya kwamba utajidhihirisha Mwenyewe, na kujionyesha Mwenyewe, usiku wa leo. Wale wanaofanya hivyo, kuwafanya watu wajiunge na kanisa, kamwe hawangetaja maneno ambayo Petro alisema katika Matendo 2, wangeogopa kutaja toba, Mungu, kuahidi ubatizo wa Roho na Roho Mtakatifu, wangeogopa kufanya hivyo, wangetupwa nje ya dhehebu lao kwa kufanya hivyo.

Mungu, tunaomba ya kwamba utawaamsha watu upesi sana na kuwajalia kuona ile saa, maana inakaribia upesi.

Sasa, tunakabidhi kila kitu Kwako sasa, upate utukufu. Nena, Baba yetu, maana tunajikabidhi pamoja na Neno Lako. Katika Jina la Yesu, Mwanao. Amina.

276 Loo, jamani! Neno, mnaliamini? Mnaamini ni Kweli? Wakati mwingine hu—huenda nikasikika kama nina hasira, bali sina. Mimi . . . Kama ungeona baadhi . . . kama ungejua nilikuwa ninashuka kwenda barabarani hapa, kuna tuta kubwa hapa chini barabarani, nawe unajua nikishuka kwenda kwenye barabara hiyo maili tisini kwa saa, nilikuwa naenda kuligonga, nilikuwa naenda, ni, nilikuwa ninaenda kuishia papo hapo, je, ungenipenda vya kutosha kunionya? Ninaamini unanipenda. Hivyo ndivyo ninavyofanya. Mnaona?

277 Mnaona, jambo ambalo . . . Kanisa linaingia katika mporomoko mkubwa sana. Mchungaji, unaona hilo, enyi kwaya, mnaona hilo, kila mtu aliye wa kiroho, ninyi watu wa kiroho mnaona hilo. Tufanyeje, jamani? Tufanyeje? Tunaliona papa hapa. Ni ninii ya mwisho . . . hakukuwako na ishara nyingine iliyomjia Ibrahimu, ama yeyote wao. Ishara ya mwisho ilipotolewa, mwana akaja. Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku hiyo, ndivyo itakavyokuwa tena katika kuja kwake Mwana wa Adamu." Je, alisema uongo? Asingeweza, Yeye alikuwa ni Mungu, asingeweza kusema uongo.

278 Sasa tutawaombea wagonjwa. Ni wangapi walio wagonjwa? Hebu tuone. (Samahani.) Inua mkono wako, wagonjwa wote walio humu ndani. (Je, uligawa kadi?) Hiyo ni afadhali, aligawa kadi kadhaa. Vema. Tutawaita. Ilikuwa—ilikuwa ni . . . ? Nini? Moja hadi mia moja? Vema. Alisema aligawa kadi za maombi A, moja hadi mia moja.

279 Vema, hebu tuwapange baadhi ya watu hawa. Ni nani aliye na A, moja? Kadi ya maombi A, moja. Iwapo huwezi kusimama, sasa, inua mikono yako, tutatuma mtu fulani akubebe. Mama huyo, waweza kusimama papa hapa? Mbili. Ni nani aliye na mbili? Ninavyowaita tu . . . Huyo mama huko nyuma, waweza kuja? Namba mbili.

280 Vema. Kadi ya maombi namba tatu, A, namba tatu. Ni nani aliye na kadi hiyo ya maombi? Namba tatu. Ni yule ndugu anayekuja pale? Vema, namba nne. Ni nani aliye na kadi ya maombi nne? Huyo mama papo hapo. Tano. Kadi ya maombi sita. Kadi ya maombi namba sita, namba saba. Vema, nane, nane, tisa, kumi, kumi. Sikuona kumi ikisimama. Namba kumi. Kumekuwa na watu walioondoka, huenda ilikuwa ni wao.

281 Kumi, kumi na moja, kumi na moja, kumi na mbili. Namba kumi na mbili, kumi na tatu, kumi na nne. Sogeza mkono wako ama kitu fulani, ili niweze kukuona upesi sana, labda. Kumi na nne, kumi na tano, kumi na tano. Kadi ya maombi namba kumi na tano, tafadhali. Kumi na sita, kumi na saba. Hiyo ni sawa. Kumi na saba, kumi na nane, kumi na tisa, ishirini.

282 Vema. Niliita wapi? Namba ishirini. Moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba, nane, tisa, kumi, kumi na moja, kumi na mbili, kumi na tatu, kumi na nne, kumi na tano, kumi na sita. Ni watu

kumi na sita tu hapo, kadiri niwezavyo kuona. Vema. Kumi na sita hadi ishirini. Moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba, nane, tisa, kumi, kumi na moja, kumi na mbili, kumi na tatu, kumi na nne, kumi na tano, kumi na sita.

283 Vema, tutaanzia hapo. (Sawa. Ni sawa.) Ni wangapi wasio na kadi ya maombi, wewe ni mgonjwa, mhitaji? Inueni mikono yenu. Kote jengoni. Vema. Ni wangapi watakaoahidi kuwa katika maombi, kwa dakika chache tu sasa, watulie tu kimya kabisa sasa, na kuwa katika maombi?

284 Nimekuwa nikihubiri kuhusu nini? Ishara ya mwisho itakayolijia Kanisa kabla ya wakati wa mwisho. Siku moja itakuwa tofauti, tutaisikia mara yetu ya mwisho. Vema. Mtakuwa ninii hasa . . .? Ni wangapi wanaoamini hilo kuwa ni kweli? Ni wangapi wanaoamini hilo? Mnaliamini, kweli? Vema. Iweni na kicho, basi, iweni na kicho kabisa, basi. Iweni tu na imani, msitie shaka.

Sasa, kama mngekuwa tu katika maombi, iweni na kicho kabisa sasa. Ninataka kuona, labda huyu mama hapa alikuwa na kadi ya maombi anayeingia katika . . .

Unayo mahali fulani kati ya moja na ishirini, Mama? (Angalia tu ni ipi, Billy, hiyo si . . .) Vema.

285 Na wakati mwingine, labda, nilisahau, mtu fulani huenda akawa ni kiziwi. Angalia kote, kama kuna kadi zingine za maombi, angalia uone, huenda ikawa ni mtu aliye kiziwi na hata asingeweza kusikia. Ni—ni—ninachelewa kidogo nami . . . Vema, hamwendi popote kesho kwa vyovyote vile, kurudi tu kanisani, sivyo? Mnaona? Hivyo tu, kwa hiyo tulieni tu sasa. Paulo alihubiri jambo lili hili usiku kucha. Hakika, alihubiri. Lakini, kwa hiyo sisi—sisi, hatuna haraka.

286 Vema, basi kila mtu awe na kicho sana sasa, na sasa msisogee huku na huku, kaeni kimya kabisa, iweni na kicho kabisa. Sasa hebu na tuinamishe vichwa vyetu, kwa muda kidogo tu.

287 Bwana Yesu, sasa ninatambua kile kinachonikabili, ninatambua ya kwamba sasa sina budi kupatikana nikisema kweli, ama kusema uongo. Sijitumainii mwenyewe, Bwana, ni—ningeogopa kufanya hivyo. Ninajua, ingawa najua ni—ni Neno Lako, nami ninajua ni Kweli, hata hivyo, Bwana, mimi . . . itakuhitaji Wewe kufanya hivyo, itakubidi kunisaidia, itakubidi kuniruhusu kufanya jambo hili, Bwana, la sivyo siwezi kulifanya, isingewezekana kabisa kwangu kufanya hivyo. Ninaomba ya kwamba Wewe utanisaidia.

288 Nibariki, nisamehe makosa yangu maishani. Bwana, mimi hapa, huku juu kabisa katika umri wa makamu sasa, laiti ningalikutumikia kutoka huko nyuma kabisa, wakati nilipokuwa mvulana mdogo, mpaka nilipokuwa, nilipoanza, yapata umri wa miaka ishirini na mmoja, laiti ningaliweza kurejesha wakati huo uliopotea, Bwana.

289 Sina budi kuja . . . Kama ungenirudisha, usiku wa leo, kuwa kijana, ningekuwa nje ya mahali pangu. Kamwe nisingeweza kuwa kijana sasa, nisingejua ninayojua, ni—nisingefufuka katika ufufuo pamoja na watu hawa ambao nimewahubiria. Sina budi kusimama katika kizazi kiki—kiki hiki kusimama kama shahidi wa Neno Lako. Kwa hiyo, Bwana, jalia niwe mkweli na mwaminifu kwa hawa watu, mwaminifu Kwako, wakati nikiwa hapa, basi, utakapomaliza nami, Bwana, mpokee mtumishi Wako kwa amani.

290 Ninaomba ya kwamba Wewe utaniongoza sasa na kunielekeza. Wabariki watu hawa, bariki kanisa hili, mchungaji huyu mzuri, mke wake, watu wote hapa, Bwana, watu wazuri, wazuri sana, ninaomba ya kwamba Wewe utakuwa pamoja nao sasa, na uwajalie waone yale ambayo ndiyo kwanza niseme, kwamba ishara za wakati wa mwisho, kila . . . huko nyuma kabisa kutoka wakati wa Nuhu, Bwana, Wewe ulitoa ishara hizo.

291 Nikiwa tu na saa moja ama mbili kujaribu kulielezea, ingekuwa ni vigumu kulielezea lote kwa utondoti, lakini ninaomba sasa, Bwana, ya kwamba Wewe utalithibitisha, hilo ndilo jambo muhimu. Lithibitishe na kuwafanya wajue ya kwamba Mungu yeye yule aliyefanya ishara hiyo huko chini mbele za Ibrahimu, Sara, na Kanisa hilo teule lililoketi huko nje jangwani, kundi dogo lisilo la kimadhehebu limeketi kule nje . . . Hawakuwa na mji wowote, walikuwa ni kundi dogo lililoishi katika mahema. Hawakuwa na majengo makubwa na vitu vikubwa vya kujitukuza, walikuwa tu ni kundi la wasafiri, bali Wewe uliwatokea, kwa sababu walikuwa na ahadi ya mwana ajaye.

292 Tunayo, pia, Baba, tunaamini hilo. Ninaomba kwamba kote kupitia Sodoma hapa, usiku wa leo . . . Tazama kote katika taifa hili. Ni visa vingapi vya uzinzi mkuu vinavyofanywa sasa? Ni nyumba ngapi zinazovunjwa? Ni dhambi ngapi zinazokuja mbele ya macho Yako sasa hivi, Bwana, katika mji uu huu? Mungu, unawezaje kulivumilia? Ninaomba uwasamehe, Bwana, hawajui wanalofanya. Kuwa karibu nasi, katika Jina la Yesu. Amina.

293 Vema. Usikivu wenu kwa muda kidogo, na hebu niangalie chini mstarini hapa kwanza. Ninaamini ya kwamba watu, kadiri nijuavyo, chini mstarini, hatufahamiani, siwajui, sijui lolote kuwahusu.

294 Kweli, kuangalia kwenye kusanyiko hapa, ninawaona marafiki wangu wazuri *pale*, Ndugu na Dada Palmer, wameketi papa *hapa* chini, kutoka Macon, ninaamini, ama, huko chini Georgia. Nami ninamjua *yule* ndugu na dada, siwezi kukukumbuka jina lao, walioketi hapo kando. Na huyu hapa,

kweli, ameketi, mtu aliyeketi papa *hapa*, Ndugu Fritzinger kutoka Ohio. Hiyo ni kweli.

295 Sasa, ninajua ya kwamba Fred Sothmann na Bibi Sothmann wako hapa, mahali fulani. Sijui ni wapi, nilimsikia akisema, "Amina," muda mfupi uliopita. Sijui yuko wapi, yuko hapa ndani mahali fulani. Na Ndugu na Dada Evans wako hapa, nafikiri. Ndugu Evans yuko, nafikiri Dada Evans yuko kambini, huko chini, usiku wa leo. Waliona hawakuwa na nafasi ya kuingia, kwa hiyo wakarudi, mke wangu, na watoto, na hao wengine. Kwa hiyo tu—tulitaka mkutano huu...Na Ndugu Tom Simpson yupo hapa, Ndugu David Wood yupo hapa, nao wananinii...Siwaoni, hata mmoja wao.

296 Lakini ni wangapi hapa ndani wanaojua ya kwamba sijui lolote kuwahusu, mna shida gani ama chochote kile? Inueni mikono yenu, kila mtu mkutanoni. Loo, ni kila mahali. Vema. Sasa, wewe amini tu, amini kwa moyo wako wote.

297 Loo, jamani! Sasa, hapa ndipo kitu kingine hakina budi kuzungumza mbali na mwanadamu, sasa, mnajua hilo. Sasa, angalieni *hapa*, angalieni mstari huu wa maombi, kila mmoja wao aliinua mkono wake, wao ni wageni. Na hii hapa mikono yangu, hii *hapa* Biblia, ni wageni kwangu, siwajui. Nami nimewaambia ni nani hasa niliyemjua huko nje, ninayeweza kumtambua kutoka kwenye jukwaa hili. Nyuma yangu, simjui mtu yeyote ila Ndugu Littlefield, kadiri niwezavyo kuona, simjui hata mmoja. *Huyu* ni Dada Littlefield? Si—sikujua kama ilikuwa ni yeye au la, sikuwa na hakika sana. Samahani kwa kuwaamsha hivi majuzi usiku hata hivyo. Kwa hiyo karibu si—simjui mtu yeyote hapa.

298 Lakini, sasa, mnaona, sasa, kama Roho Mtakatifu yuko katika Neno, Neno lililoahidiwa, basi Yeye aliahidi, katika siku za mwisho, kutoa ishara ya Kimaandiko kabla tu ya kuja kwa Mwana wa Adamu, kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma. Hiyo ni kweli? Sasa, hivi hamwamini, ndugu mlio miongoni mwetu, ya kwamba kundi hili dogo la watu ndilo lile kundi lililoitwa litoke? Hivi hamwamini ka—kanisa la Kipentekoste, katika hekaheka zake zote, ninaamini mle ndani kuna lile kundi la watu walioteuliwa, walioitwa watoke, ninaamini hilo. Hakika, hakika.

299 Si wote walio katika ulimwengu wa Kipentekoste, lakini ninamaanisha, katika hilo—katika kundi hilo, wako mle ndani mahali fulani, sijui mahali walipo, lakini wako mle ndani mahali fulani, maana hakutakuwako na wakati mwingine wa kanisa, huu ndio wa mwisho. Lakini Mungu atamchukua huyo Mteule kutoka kwenye kundi hilo la Kipentekoste, na kulichongea katika lile Jiwe lijalo kama tu...ambalo ingebidi litoshee namna hiyo lipate kulishushia Paa hiyo. Hebu angalieni, halitakuwa kombo, na kukaa *hivi*, litaenea kikamilifu. Nalo

Kanisa hili litalazimika kuwa na huduma iyo hiyo, naye Yesu alishuhudia jambo lilo hilo.

300 Sasa, tunaanzia wapi? Je, *huyu* ndiye mtu wa kwanza, ama *yule*? *Huyu* hapa? Vema, Mama, simama tu mahali ulipo ukitaka, si lazima usonge mbele zaidi.

301 Sasa, sisi hapa, mwanamume na mwanamke tukikutana hapa, kama tu vile Yesu alivyokutana na yule mwanamke kisimani. Sijawahi kumwona, sijui lolote kumhusu, yeye ni mwanamke tu aliyesimama hapo, ndiyo yote nijuayo, nanyi ni watu huko nje. Sasa, nina ninii . . . Sasa, angalieni, kwa namna fulani anaonekana mwembamba, lakini kwa kweli angeweza kuwa mwanamke mzuri, mwenye afya, mwenye nguvu, huenda akawa, huenda amesimama hapo kwa ajili ya mtu mwingine, sijui, sijawahi kumwona. Lakini sasa, kama Roho Mtakatifu . . .

302 Kama ningeweza kumponya, ningetembea kule . . . Kama yeye ni mgonjwa, tuseme kwa mfano, tuseme, vema, mwanamke mwembamba ungewazia TB. Vema, tuseme alikuwa na TB, ningeenda pale na kusema, "Nitakuwekea mikono, Dada. Mungu asifiwe, ninakuponya katika Jina la Yesu." Kama mimi . . . Kama Bwana angeniambia niende nikafanye hivyo, ningeenda, ningeenda nilifanye. Mnaona? Lakini sitaenda kule na kusema jambo hilo mpaka Yeye aniambie niliseme, maana silijui.

303 Mtu fulani alikuja na gari mbele ya nyumba hivi majuzi tu, kundi zima la watu huko nje, naye akasema, akamwambia mke wangu, nilikuwa tu ndio kwanza niingie ndani, kasema, "Hebu tu Ndugu Branham aje mlangoni na kuniambia binti yangu atakuwa mzima. Hivyo tu ndivyo anavyopaswa kufanya, aje tu na kuniambia."

Meda akasema, "Vema, nenda huko nje na . . . "

304 Nikasema, "Vema, ningefanya nini? Kama ningeenda nimwambie, bila kujua, ningekuwa nikidanganya." Nikasema, "Kama Bwana angeniambia niende nikamwambie hivyo, ningeenda nimwambie hivyo, lakini mpaka aniambie hivyo, siwezi kusema zaidi ya yale anayoniambia niseme." Hivyo ndivyo ilivyo, kwenda tu ukidhania uko sawa, lakini hilo—hilo ni kosa, huwezi kulidhania. Wewe . . .

305 Na papa hapa huwezi kudhania, siwezi kusema, "Nadhani mwanamke huyu anamwombea shangazi yake mgonjwa." Hilo halitafaa kitu, angejua vizuri zaidi. Vema, huenda anafanya hivyo, mnaona, lakini ninamaanisha, kulidhania tu, mnaona, huwezi kufanya hivyo, haina budi kuwa ni kweli, haina budi kuwa ni kweli. Na hapa ndipo inapobidi kuthibitishwa kama ni kweli ama si kweli.

306 Sasa, kumbukeni, hebu kila mtu akumbuke, mimi ni ndugu yenu, mnaona, mwanadamu tu. Lakini—lakini karama ya Mungu, nikiamini Ujumbe huu, na kuamini Yeye alinituma kuhubiri Ujumbe huu, kisha nikijitolea kwa Roho Mtakatifu,

na Neno hilo mle ndani liko moyoni mwangu, na, "Mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu ndani yenu, ombeni mtakalo." Si, Kaeni, sio kukimbia tu na kuruka kutoka *hapa* hadi *pale*, lakini "Mkikaa ndani Yangu, Neno Langu ndani yenu, ombeni mtakalo." Hiyo ni kweli?

307 Sasa, ningependa tu kuzungumza nawe kwa dakika moja, Mama, nimekuwa nikihubiri, kwa dakika chache tu, wakati tu mkisimama papo hapo, kusudi tu niweze kuwatenga na mtu mwingine. Na kama tu vile Bwana wetu alivyozungumza na yule mwanamke kisimani, mwajua, Alikuwa tu akiishika roho yake, mpaka akagundua shida yake ilikuwa ni nini, ndipo alipopata shida yake, alimwambia shida yake ilikuwa ni nini, naye akasema hiyo ilikuwa ni ishara ya Masihi. Vema, kama Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele, halafu basi, unanijua, kama mwanadamu, nisingeweza kufanya hivyo, na kama ingefanywa tena, hiyo si ingekuwa ndiyo ishara ya Masihi tena? Mngeamini hilo, enyi Kanisa?

308 Sasa, kuzungumza tu naye kwa dakika moja sasa, mnaona. Si mimi, Masihi; bali Masihi akinena kupitia kwangu. Mnaona? Jambo ndilo hilo, maana simjui, sijawahi kumwona. Sasa, kama tukipata...Hebu kidogo, mpaka mimi...sijui jinsi atakavyolifanya, huenda hata asilifanye.

309 Naam, huyu mama hana budi kupata usaidizi sasa hivi, la sivyo atakufa, ana kansa. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Ili watu wajue, inua mkono wako namna *hiyo*. Unataka nikwambie iko wapi? Iko kooni. Hiyo ni kweli. Unaamini kwa moyo wako wote? Basi utakubali...? [Dada huyo anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Vema, sasa, angalia, sasa, unasema unaamini ya kwamba Yeye anaweza kukuponya, basi kulingana na Biblia Yeye amefanya hivyo, kama unaamini hilo. Sasa, hilo Neno ni kweli? Basi umeponywa, sivyo? Hiyo ni kweli. Amina. Shuka uende ukaseme, "Asante, Bwana," na usahau yote kuuhusu, na upate afya. Amina.

310 Hatufahamiani mmoja kwa mwingine. Sikujui, kwa kweli sijawahi kukuona, nadhani, hatufahamiani, tumekutana tu hapa. Lakini Mungu anatujua sote wawili, mnaamini hilo, sivyo? Biblia ilisema, "Yeye aaminiye..." Iweni tu na kicho kabisa. Kama Bwana Mungu anaweza kuniambia...Kama nikienda pale na kusema, "Mama, wewe ni mgonjwa." Sasa, huenda ukawa mgonjwa, ukisimama hapo kwenye mstari huo wa maombi, huenda hiyo ni kweli. Na huenda ikawa umesimama hapo kwa ajili ya mtu mwingine, sijui. Lakini kama ungekuwa mgonjwa, nami nilitaka kwenda kukuwekea mikono, niseme, "Yesu alisema, 'Ishara hizi zinafuatana na hao waaminio, wakiweka mikono juu ya wagonjwa, watapata afya.'" Hiyo ni kweli.

311 Lakini ngoja kidogo, hebu na tuthibitishe kama Yeye

alimtuma mtu huyo au la. Mnaona? Hebu tuone kwanza, mnaona, kama itafanya kazi hivyo au la. Mnaona? Kumbukeni hilo. Hayo maneno mawili, kwa kudhania, huja kwa wawili... Daima imekuwa ninii...Shetani alijaribu kuifanya kazi ya Mungu katika...Neno la Mungu litende kazi katika bustani ya Edeni kwa kulipaka chokaa. Moabu walijaribu kufanya vivyo hivyo. Shetani alifanya jambo lile lile mbele za Yesu, akamrukia kwa elimu yake ya kikanisa na maarifa, na kusema, "Imeandikwa, imeandikwa."

312 Yesu alimrukia tena moja kwa moja, kasema, "Pia imeandikwa." Lingefanya kazi kwa Yesu. Kwa nini? Neno lilikuwa katika Neno, hilo ndilo lililolifanya litende kazi. Umeme ulikuwa kwenye Waya, hiyo ndiyo tofauti.

313 Sasa, inahitaji umeme katika waya hapa. Mnaona? Mimi ni waya tu, lakini Yeye ndiye Umeme, kwa hiyo waya umekufa bila ya Umeme. Kwa hiyo kama huo Umeme ni wa Mungu, Roho Mtakatifu, anaweza kupitia kwenye waya, ndugu yako, na anaweza kukuelezea, ama kwa Roho Mtakatifu, kama alivyomwelezea yule mwanamke kisimani, kuelezea jambo fulani ambalo umefanya, ama jambo fulani ulilopaswa kufanya, ama—ama kitu ambacho—ambacho ni cha wakati uliopita, ambacho wewe...utajua kama ni kweli ama si kweli, ama kama wewe ni mgonjwa, una shida fulani, aseme shida yako, ndipo u—ungejua kama hiyo ni kweli ama si kweli, sivyo? Ungejua jambo hilo. Hiyo ni kweli, enyi Kanisa?

314 Basi kama anaweza kukwambia yale yamekuwako nawe unajua kama hiyo ni kweli ama si kweli, basi kama akikwambia yatakayotukia, unajua ni kweli. Unaona? Na tayari unajua yatakayotukia, kama Yeye—kama Yeye aliyasema papa *hapa* katika Neno Lake. Si lazima litoke kwangu, tayari limekuja, jambo pekee ni thibitisho sasa, ya kwamba *Hili*, Neno hili, imani yako, utu wako, na Neno la Mungu vinakutana pamoja papa hapa. Unaona? Mimi ni msemaji tu wa kuhamisha. Unaona?

315 Hii *hapa* ahadi ya Mungu, Mungu alisema hii ingekuwa ndiyo ishara ya siku ya mwisho. Hizi hapa siku za mwisho hapa, tunaishi ndani yake. Vema. Sasa, ni kweli? Huyu hapa Roho Mtakatifu amesimama sasa, sasa hivi. Ni wangapi waliopata kuona ile picha ya yule Malaika kwenye ile...Nuru ile? Mnaona? Yuko papa hapa, sasa hivi. Yuko papa hapa, papa hapa ninaposimama. Huyo ndiye hasa anayezungumza, Hilo ndilo hasa linalomfanya mwanamke huyu. Mnaona?

316 Huyu nwanamke ana shida na masikio yake, ana shida na masikio yake. Hiyo ni kweli. Hupata shida kidogo ya kusikia pia, nayo. Hiyo...Inua mkono wako, kama hiyo ni kweli.

Sikuzote mimi hushika hilo, mtu fulani anafikiri ninababahatisha hilo. Unadhania vibaya, sibahatishi hilo.

317 Angalia tu kwa dakika moja. Nataka tu kuzungumza nawe. Sasa, hebu tuone, sijui Yeye alisema nini. Chochote kile, kilikuwa sahihi. Naam, ni masikio yako, naona sasa, kuna kitu kinachoenda mrama masikioni mwako. Nawe una shida fulani kichwani, ni kama kuumwa na kichwa, kama kipandauso ama kitu fulani, unakaa . . . Hiyo ni kweli, sivyo? Um-hum.

318 Isitoshe, bali, bali unamwombea mtu fulani, una mtu fulani pamoja nawe usiku wa leo. Hiyo ni kweli. Yeye ni mwa—mwanamke, mwanamke mzee, hiyo ni kweli kabisa. Anaumwa na masikio yake pia. Ninamwangalia moja kwa moja sasa, nikikuangalia. Naam, bwana. Kitu kingine alicho nacho, ana shinikizo kuu la damu, ana yabisi kavu. Hiyo ni kweli. Um-hum. Hiyo ni kweli kabisa. Vema. Ruby, unaamini atapona? Unaamini atapona? Unaamini utapona, Bibi Crumley? Ruby Crumley. Rudi ukawaambie hiyo ni kweli.

319 Unaamini? "Kama unaweza kuamini!" Sasa, amini tu. Sasa, kuita jina lake hakukuwa kitu. Hivi Yesu hakumwambia Petro, "Jina lako ni Simoni, baba yako alikuwa Yona"? Mnaona, ni, mnaona, bado ni Yeye tu.

320 Sikujui, Bwana, hatufahamiani mmoja kwa mwingine. Lakini unaamini ya kwamba Mungu anaweza kunifunulia shida yako? Je, ungeniamini mimi kuwa mtumishi Wake kama ningefanya hivyo?

Je, kusanyiko, kila mtu humo ndani angeamini jambo lile lile?

321 Jambo fulani lilitukia. Si katika kusanyiko. Sikulipata tu vizuri. Hebu nishike ninii wenu, usikivu wenu tu tena, kwa muda kidogo tu. Uko hapa kwa ajili ya mtu mwingine. Mtu huyo hayupo hapa, hawako katika mji huu, hata hawako katika jimbo hili, wako Carolina. Hiyo ni kweli. Ni mke wa mhudumu, naye ana kansa, hiyo kansa iko kwenye titi, unasimama kwa ajili yake. Unaamini atakuwa mzima? Yesu Kristo na awajalie hili, yale hasa mliyoomba.

U hali gani? Hatufahamiani. Lakini unaamini Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, yu hai usiku wa leo?

322 Ndio kwanza inaanza kwenye kusanyiko sasa. Kidogo ni vigumu kuishikilia hapa jukwaani. Inaninii tu—inaendelea tu, inaenea kote katika kusanyiko. Mnaona? Laiti mngeweza kuamini, enyi marafiki, sasa hivi, mngeona Roho wa Mungu akianza kutenda kazi. Nitajaribu kuweka usikivu wangu huku kadiri niwezavyo kwa watu hawa niliowaweka mstarini.

323 Wewe ni mgeni, pia. Hiyo ni kweli. Umekuwa hospitalini, ulifanyiwa upasuaji, ugonjwa wa uti wa mgongo. Hiyo ni kweli. Unataka kurudi Georgia ukawe mzima? Sasa, unataka? Bibi Colleen? Rudi chini na uamini kwa moyo wako wote na uwe mzima.

324 Vipi kama ningekwambia ugonjwa wako wa mgongo umepona, ukisimama hapo? Je, ungeniamini? Vema, rudi ukaudai tu, useme, “Asante, Bwana.” Nenda ukiamini.

Nawe una jambo lile lile. Nenda tu ukaamini, hilo tu ndilo unalopaswa kufanya.

Ugonjwa wako wa tumbo? Nenda, ukale. Yesu Kristo anakuponya, hakika, kama ukiamini kwa moyo wako wote.

Una ugonjwa wa wasiwasi, unakupa ugonjwa wa tumbo, pia, kwa hiyo endelea tu moja kwa moja ukale chakula chako cha jioni.

Unaamini kwa moyo wako wote? Amini.

325 Ugonjwa wa moyo si kitu kwa Mungu kuponya. Unaamini Yeye atakuponya? Rudi kitini, na useme, “Asante, Bwana, kwa kuniponya.” Hiyo ni kweli.

326 Hupandi *huko* juu, maana yabisi kavu inaumiza, bali Mungu anaweza kuiponya. Unaamini hilo? Rudi moja kwa moja, na useme, “Asante, Bwana,” na upone.

Wasiwasi ni jambo kuu, bali unaamini Mungu anaweza kuponya wasiwasi wako? Rudi na useme, “Asante, Bwana,” na upate afya.

Unaamini kwa moyo wako wote, kila mtu? “Kama unaweza kuamini . . . ”

327 Vipi kama sikukwambia jambo, na kukwambia tu utakuwa mzima, na moyo wako . . . Vema, endelea, umeponywa haidhuru, kwa hiyo ninii tu . . . nilisema hayo hapo kabla na . . .

328 Sasa, kwa muda mrefu jambo hili limekuwa likikusumbua, unaona, na kuchacha tumboni mwako na kadhalika namna hiyo. Unaamini Yeye atakuponya sasa? Nenda, ukale. Asante. Uwe mzima.

Je, kila mtu anaamini kwa moyo wako wote?

329 Maskini huyu mama aliyeketi hapa ameinamisha kichwa chake, aliyeketi papa hapa ndani, anaomba. Kuna mwanamke aliyeketi karibu naye hapo, sijui jina lake, sijui yeye ni nani. Lakini mtu huyo anamwombea mpendwa apate kuokolewa. Hiyo ni kweli kabisa. Kama utaamini kwa moyo wako wote ya kwamba Mungu atawaokoa, nenda, na Mungu atakupa sawasawa kabisa na kujibu maombi yako. Jina la huyo mama, aliyeketi hapo ni nani? Siwezi kuona, wewe uliyeketi papo hapo karibu naye. Naam. Mwambie aamini, Mungu amejibu maombi yake. Amina. Bwana asifiwe. Amina.

Unaamini? Usiwe na shaka, mwamini Mungu.

330 Fran Sothmann, wewe ndiwe uliyeketi hapo nyuma, ninayekuangalia? Weka mkono wako juu ya mwanamke huyo karibu nawe hapo, rafiki yako aliyeketi hapo. Ana ugonjwa wa figo. Unaamini utaponywa, Mama? Vema, bwana.

Mume wako ameketi hapo karibu, ana tatizo la macho yake. Unaamini ataponywa? Weka mikono yako juu yake. Wote wawili hatufahamiani. Sijawahi kuwaona maishani mwangu. Unaamini kwa moyo wako wote? Yesu Kristo anakuponya. Amina.

Unaamini?

Mungu anaweza kuponya ugonjwa wa tumbo, matumbo ya wasiwasi. Unaamini hilo? Akupe afya? Basi upokee. Yesu Kristo anakuponya. Amina.

331 Ni wangapi hapa ndani mnaoamini kwa moyo wenu wote? Juu na chini, juu na chini. Mnaamini Huyo ni Bwana Mungu yeye yule aliyesimama pamoja na Ibrahimu kule chini siku ile, akajiwakilisha Mwenyewe katika mwili wa kibinadamu? Hivi hamwoni ni Mungu yeye yule ndani yenu, Mungu yeye yule ndani yangu, ishara ile ile aliyotoa kabla tu ya wakati wa mwisho kwa Kanisa teule? Hivi hamwamini hilo? Hivi hamwamini hiyo ni. . . Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele? Hivi hamwamini hiyo ndiyo ishara ya Yeye kuja? Hivi hamwamini ishara hiyo, hivi karibuni ulimwengu utaangamizwa, na ule Utawala wa Miaka Elfu utaanza, tutakuwa na utawala mkuu pamoja na Mungu? Hivi hamwamini hilo? Ni ishara za wakati wa mwisho.

332 Ni wangapi Uzao wa Ibrahimu walio hapa ndani, usiku wa leo, wakiwa na tumaini hilo ndani yao, wakitulia katika Mungu? Yesu Kristo Mwana wa Mungu alisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao Wazao wa Ibrahimu, hao waaminio." Je, wewe ni mwaminio? Inua mkono wako. Sasa, sijali una shida gani. Hilo halimaanishi kitu, mnaona, kuwaambia tu, na kufunua, mnaona, hiyo inahitaji imani yako kuponya, unaona. Imani yako hufanya hivyo. Unaona? Imani yangu katika karama ya Mungu ndiyo inayolifunua, kwa sababu Mungu alitoa ahadi, ndipo Mungu akanifunulia hiyo ahadi kupitia Neno Lake, nami ninadumu na ahadi hiyo. Mnapata ninalomaanisha? Ninadumu pamoja na ahadi hiyo.

333 Maskini mama huyo aliyeketi hapo na ugonjwa huo wa kibofu, unaamini Mungu atakuponya? Vema, bwana, nawe unaweza kupata shauku yako. Mungu akubariki. Sasa, wewe, una wasiwasi kuhusu kadi yako ya maombi? Haikubidi kuwa na wowote, hata hivyo, unaona, Mungu alikuponya.

334 Sasa, hivi hamwoni ninalomaanisha? Ni kila mahali tu. Mnaamini hilo? Wekeaneni mikono. Ombeaneni tu, nitawasikiliza. Ombeaneni, wekeni mikono mmoja juu ya. . . Ninataka kuona jinsi mnavyoomba.

335 Wekeaneni mikono, hapa katika kundi hili dogo hapa linalosimama kwenye mstari wa maombi, weka. . . geukeni, geuzianeni mikono, weka mkono wako, sasa ombeaneni. Ninii tu, ninataka kuwasikia mkiomba. Vema.

336 Usijiombee sasa, mwombee yule uliyemwekea mikono. Jambo ndilo hilo. Mnaosimama nje ukumbini, kila mahali, wekeaneni mikono.

337 Baba yetu wa Mbinguni, tunauleta mkutano huu kwenye wakati huu mkuu wa upeo. Ibilisi angefanya kila awezalo kuuzuia, lakini, Mungu, umejionyesha upo, Uwepo wa Roho Mtakatifu kwa Neno, kwa ishara za Kimaandiko, kwa Biblia Yenyewe, inayotoa ahadi, na kusema mambo haya yangetimia katika siku za mwisho.

338 Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, Yeye ajuaye mioyo, majina, kila kitu, magonjwa, na yaliyokuwako, yaliyopo, na yatakayokuwako, Wewe unajua yote kuyahusu, na watu hawa walioketi hapa ni watu Wako, wao ni watoto wa Mungu, nao wanakuamini Wewe, wamewekeana mikono, Ulisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio, wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya."

339 Sasa, ninaweka maombi yangu pamoja na yao, ninaamini pamoja nao, ninaamini ya kwamba kile wanachokuomba Wewe utawapa, kwa sababu wao ni watoto Wako, hutawanyima chochote chema hao waendao kwa unyofu mbele Zako.

340 Sasa, Shetani, tunakuja kwenye wakati huu kukupa changamoto. Umeshindwa, umeshindwa tangu Kalvari, hakuna kitu ulicho nacho unachoweza kutoa, ila udanganyifu, nasi hatukuachi kudanganya tena. Tunaweka Neno la Bwana Mungu, Neno la Bwana lilisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Watu hawa wanakiri kuwa na ubatizo wa Roho Mtakatifu. Wamehisi nguvu za kimbinguni za Mungu zikiingia ndani yao kubadilisha maisha yao, wanahurumiana, wanaombeana.

341 Loo, Shetani, ewe mwovu, ambaye umewafanya watu hawa wagonjwa, tunakuapisha, katika Jina la Yesu Kristo, waachilie watu hawa, toka ndani yao. Katika Jina la Yesu Kristo, waachilie. Toka, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

342 Simameni kwa miguu yenu sasa. Simameni, mpeni Mungu sifa. Inueni mikono yenu hapa ndani. Sijali kama wewe ni kiwete, simama haidhuru. Inueni mikono yenu na mumpe Mungu sifa.

62-0407 Ishara Za Kuja Kwake
Church Of Faith
Cleveland, Tennessee Marekani

SWAHILI

©2026 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org